
# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI KWA MIAKA MIWILI 2015 – 2017, JIMBO LA ILEMELA, MKOA WA MWANZA




**KAULI MBIU YA JIMBO**

**"ILEMELA NI YETU TUSHIRIKIANE KUIJENGA"**

# TANZANIA MPYA CCM MPYA



***"NIMEAMUA NCHI IENDE NA ITAENDA,***

***ANAEDHANI ATANIKWAMISHA ATAKWAMA YEYE***

***KWA KUWA HATA MUNGU YUKO PAMOJA***

***NA MIMI "***

***Dr. John Pombe Joseph Magufuli,***

***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2017***

## YALIYOMO


1.0 Utangulizi----------1
- Eneo La Jimbo----------1
- Mahali Jimbo Lilipo----------1
- Ramani Ya Wilaya Ya Ilemela (Jimbo La Ilemela)----------2

1.1 Hali Ya Kisiasa----------3
1.2 Ahadi Za Mbunge Na Utekelezaji Wa Ilani Ya Uchaguzi----------3
2.0 Shughuli Za Maendeleo Zilizotekelezwa Kwa Kipindi Cha Miaka Miwili 2015 – 2017----------4
2.1 Sekta Ya Kilimo Na Ushirika----------4
2.2 Sekta Ya Mifugo Na Uvuvi----------5
2.3 Viwanda Na Biashara----------7
3.0 Uwekezaji ----------10
4.0 Sekta Ya Ardhi, Nyumba Na Maendeleo Ya Makazi----------11
4.1 Mafanikio katika sekta ya ardhi----------16
5.0 Sekta Ya Ujenzi Na Uchukuzi----------18
5.1 Viwanja Vya Ndege----------18
5.2 Ufunguzi Wa Barabara Kale----------18
5.3 Pesa Za Mfuko Wa Barabara----------20
5.4 Uimarishaji Barabara Za Tanroad Na Halmashauri----------23
5.5 Madaraja----------23
5.6 Vivuko----------25
6.0 Nishati----------25
7.0 Mawasiliano----------27
8.0 Huduma Ya Afya----------27
8.1 Mafanikio Ya Sekta Ya Afya----------28
8.2 Ujenzi Wa Hospitali Ya Wilaya----------30
8.3 Ujenzi Wa Miundombinu Ya Kituo Cha Afya Karume----------31
8.4 Upatikanaji Wa Dawa Muhimu----------32
8.5 Matukio Ya Kijamii----------32
9.0 Elimu, Sayansi Na Teknolojia----------37
9.1 Shule Za Msingi----------38
9.2 Elimu Sekondari----------39
10.0 Maji----------47
10.1 Changamoto----------53
11.0 Uwezeshaji Wa Wananchi Kiuchumi----------54
11.1 Elimu Ya Ujasirimiamali----------54
11.2 Utoaji Mikopo Kwa Wanawake Na Vijana----------58
11.3 Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake----------58
11.4 Mafanikio Ya Mpango----------59
11.5 Uboreshaji Wa Maisha.----------59
12.0 Ujenzi Wa Chama----------61
12.1 Ushiriki Katika Vikao Vya Chama----------61
12.2 Ushirikiano Na Chama Na Wanachama----------61
12.3 Michango Na Uwekezaji Katika Chama----------61
13.0 Hamasa Na Michezo----------61
14.0 Mahusiano Na Jamii----------69
15.0 Ziara Mbalimbali Katika Jimbo----------70
16.0 Ushiriki Wa Shughuli Za Maendeleo----------72
17.0 Uwezeshaji----------72
18.0 Ofisi Ya Mbunge----------73
19.0 Kauli Mbiu Ya Jimbo----------74
20.0 Mawasiliano----------74
21.0 Changamoto----------74
22.0 Shukurani----------74
23.0 Matarajio----------74
24.0 Hitimisho----------72

## 1.0 UTANGULIZI

Jimbo la Ilemela ni kati ya Majimbo tisa ya uchaguzi kwa Mkoa wa Mwanza, lina tarafa moja, Kata 19 ambazo ni Kata ya Kirumba, Kitangiri, Nyamanoro, Ibungilo, Pansiasi, Kawekamo, Ilemela, Kiseke, Nyasaka, Buzuruga, Mecco, Nyakato, Nyamhongolo, Buswelu, Kahama, Shibula, Bugogwa, Sangabuye na Kayenze; na mitaa 171 na Matawi ya CCM ni 125.

Taarifa hii ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ni ya miaka miwili 2015 – 2017 tangu nichaguliwe kuwa Mwakilishi wa wana Ilemela kwa nafasi ya Ubunge. Vilevile, utekelezaji wake pamoja na kuzingatia mambo muhimu yaliyoanishwa kwenye Ilani ya uchaguzi, umegusa pia baadhi ya ahadi zilizotolewa na Mhe Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae pia ni mlezi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Aidha ahadi zote zilizotekelezwa na zile zinazoendelea kutekelezwa zitaonekana katika katika ***majedwali namba 1 – 6*** katika taarifa hii.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru baadhi ya wadau waliofanikisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo Jimboni. Mafanikio yote yaliyopatikana yametokana na ushirikiano mzuri kati ya Mbunge, Katibu wa Mbunge, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Waratibu wote katika Ofisi za Mbunge za Kanda, Waheshimiwa Madiwani, wapiga kura wangu ambao wamesababisha utekelezaji wa majukumu yangu kuwa mwepesi. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali waliochangia kwa hali na mali kupatikana kwa mafanikio haya ndani ya kipindi kifupi, kwa kuwezesha kufanyika shughuli za maendeleo kwa ufanisi mkubwa. Wakati huohuo naishukuru sana ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambayo iliwezesha shughuli zote zifanyike katika hali ya usalama zaidi.

### - ENEO LA JIMBO


Jimbo linaukubwa wa kilometa za mraba zipatazo1,080 kati ya hizo kilometa za mraba 828 sawa na asilimia 76.6 zimefunikwa na maji na kilometa za mraba 252 sawa na asilimia 22.4 ni nchi kavu.

### - MAHALI JIMBO LILIPO

Jimbo la Ilemela linapatikana katika latitude 2°15’ na 2°31’ Kusini mwa mstari wa Ikweta na longitude 32°45’na 33° Mashariki mwa grinwichi. Jimbo liko kusini mwa Ziwa Victoria, Magharibi limepakana na ziwa Victoria, Mashariki limepakana na Jimbo la Magu na Kusini Jimbo la Nyamagana.

# RAMANI YA WILAYA YA ILEMELA

## (Jimbo la Ilemela)



### 1.1 HALI YA KISIASA.

Hali ya kisiasa katika Jimbo ni shwari, vyama vyote vinafanya shughuli zake na vyote vyenye wawakilishi vimeungaishwa pamoja na jukwaa la TCD (Tanzania Center for Democras). Katika uchaguzi wa Mwaka 2015, wananchi wa Jimbo la Ilemela walishiriki kuwachagua viongozi wao kwa ngazi zote, yaani uchaguzi wa Rais, Mbunge na Madiwani. Kupitia uchaguzi huo wananchi wa Jimbo la Ilemela walimwamini na kumchagua Dkt. Angeline S. L. Mabula wa CCM kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilemela kwa jumla ya kura 89,289 sawa na asilimia 59.33% dhidi ya mshindani wake wa karibu Ndugu Highness Kiwia wa CHADEMA aliyekuwa anatetea nafasi hiyo na ambae alipata kura 59,596 sawa na 39.60%.

Pamoja na matokeo hayo, ndugu Highness Kiwia alifungua shauri Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza ya kupinga matokeo kupitia shauri Misc. Civil case No. 2 ya 2015, ambapo alishindwa kesi hiyo na kuamriwa alipe gharama zote. Nilifungua charge kumtaka anilipe gharama, Misc. Civil Application No. 7 ya 2016 katika Mahakama kuu kanda ya Mwanza Kesi hiyo ilisimamamiwa na wakili mzoefu *Mhe Wakili M.J. LUGAZIYA, hadi leo hii Ndugu Kiwia hajalipa madai yangu.* Kwa hakika kesi hii ilinipotezea muda mwingi wa kuwatumikia wananchi kwa ufanisi pamoja na gharama kubwa za fedha zilitumika kuweka wakili kusimamia kesi hiyo.

### 1.2 AHADI ZA MBUNGE NA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA MWAKA 2015 – 2020

Niwazi kuwa unapokuwa Mgombea kuwakilisha Chama katika Uchaguzi wowote, mara nyingi mambo yanayoahidiwa kutekelezwa hutokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama kinachoshiriki uchaguzi. Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020 imeandikwa kwa kuzingatia mambo makuu yafuatayo;

- Kuendelea kushika dola kwa kuwaongoza Watanzania kwa njia ya kidemokrasia.
- Utekelezaji wa Ilani kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, na mwelekeo wa Sera za CCM zenye lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi.
- Kuondoa umaskini wa kipato.
- Kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.
- Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.
- Kuendelea kudumisha Amani, Ulinzi na Usalama wa maisha ya wananchi na mali zao

Pamoja na mambo hayo ya msingi, kama mgombea kuna ahadi nilizotoa kwa wananchi ambazo zinarandana na yale yaliyoorodheshwa katika Ilani ya uchaguzi 2015 – 2020. Aidha, utekelezaji wake kwa sehemu kubwa umefanikiwa kutokana na ushirikiano wa dhati na wadau mbalimbali wa maendeleo. Ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni ni pamoja na zifuatazo:

1. Kuboresha miundombinu ya Elimu ili kuweka mazingira mazuri ya kufundisha na kujifunzia;
2. Kuboresha mazingira katika vituo vya afya na zahanati na kuongeza ama kuanzisha nyingine mpya;
3. Kuanzisha mashindano mbalimbali ya michezo ikiwemo Jimbo cup, muziki n.k ili kuibua vipaji kwa vijana;
4. Kusogeza huduma ya maji hasa katika maeneo yenye ukosefu kubwa ya maji kwa kushirikiana na MWAUWASA na wadau mbalimbali;
5. Kuboresha miundo mbinu ya barabara ikiwemo kufufua barabara zilizokuwa zikitumika enzi za ukoloni na kufungua barabara mpya;

6. Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa Wanawake na Vijana

7. kusimamia kwa karibu kutengwa kwa 10% ya kila mwezi katika Mapato ya ndani ya Halmashauri na kuwawezesha vikundi mbalimbali vya Wanawake na vijana kupata mikopo;

8. Kuboresha mazingira ya wauza kahawa katika mitaa yetu;

9. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zote za Mhe Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu za Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan.

10. Kuboresha vituo vya Polisi ikiwemo ukamilishaji wa nyumba ya askari Kata ya Kiseke na kituo cha Polisi Kata ya Ilemela

11. Kuweka umeme katika Jengo la Kituo cha Polisi Kata ya Bugogwa lililopo mtaa wa Kigote kwa kushirikiana na Kata husika; na

12. Kuboresha mazingira ya kazi kwa waendesha bodaboda.

## 2.0 SHUGHULI ZA MAENDELEO ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI 2015 – 2017 KWA MUJIBU WA ILANI YA UCHAGUZI NA AHADI ZA VIONGOZI.

### 2.1 SEKTA YA KILIMO NA USHIRIKA

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 22 (a) | Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa hususani katika kuboresha mifumo ya utoaji wa ruzuku na pembejeo pamoja na kuwaunganisha wakulima na Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Taasisi nyingine za Fedha. | ❖ Jumla ya tani 29 za mbolea ziligawiwa kwa wakulima, pia tani 12 za mbegu bora za mahindi zilisambazwa kwa wakulima. Vilevile Wakulima 147 walifundishwa matumizi ya teknolojia ya kisasa na zana za kilimo kupitia wataalam wa kilimo wa Kata na Mitaa.<br>❖ Wakulima 340 walifundishwa mbinu za kilimo na Kanuni za Kilimo bora kupitia Wataalam wa Kata na Mitaa.<br>❖ Jumla ya mashamba darasa 12 ya wakulima yalianzishwa ili kuonesha kanuni za kilimo bora kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali. |
| 22 (e) | Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa kuendelea kupima mashamba ya wakulima na kutoa hati milki za kimila kwa wakulima wadogo kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi na kutumia hati hizo kama dhamana ya kupata mikopo. | Bonde moja la Nyamadoke limepimwa na hatua ya kupanda vigingi kuonyesha mipaka imekamilika kwa baadhi ya maeneo na maeneo mengine kazi bado inaendelea. |
| 22 (f) (i) | Kuainisha na kupima maeneo ya ardhi ya kilimo ili kuwawezesha wakulima kujiajiri katika sekta ya kilimo hususan kilimo cha mazao ya mbogamboga, matunda, maua, mbegu za mafuta na nafaka. | Jumla ya hekta 250 za mashamba zilipimwa kwa ajili ya bustani, katika eneo la mabonde katika eneo la Nyamadoke |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 22 (f) (iii) | Kuwaunganisha wakulima (vijana na wanawake) na asasi za Fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya pembejeo, zana bora na mashine za usindikaji kupitia vyama vyao vya ushirika na vikundi vya uzalishaji mali. | Jumla ya vikundi 6 vya wakulima kwa mchanganuo wa Vijana vikundi 3 na Wanawake vikundi 3 vimepewa mikopo ya kilimo. Vikundi hivyo ni Umoja wa vijana Buyombe, Victoria B, Kayenze, Majiko sanifu Nyamhongolo, (Wanawake), Mshikamano Shibula (Wanawake), Songambele Buswelu (Wanawake) na Bugogwa kikundi cha vijana wa bustani. |
| 22 (g) (iv) | Kuviimarisha na uviwezesha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kwa kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na biashara. | Jumla ya vyama vya ushirika 10 vimewezeshwa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kupitia mfumo wa uchambuzi wa masoko. Vyama hivyo ni; Wauza Samaki Mwaloni, Ibanda Fisheries Dealers, Mwakiyo, Wasatu, Vijana Wanunuzi na Wauza Samaki, Mkombozi Fish Supply, UWASA, Nguvu Moja Wazazi, Tupendane Matunda Mwaloni na Wauza Samaki Tushirikiane Mwaloni |
| | Kuwezesha wakulima kupata elimu ya matumizi ya teknolojia rahisi ya uhifadhi wa chakula | Jumla ya wakulima 166 kutoka Kata 6 za Kayenze, Sangabuye, Shibula, Kahama, Buswelu na Bugogwa Wamepata elimu ya matumizi ya teknolojia rahisi ya uhifadhi wa chakula kupitia Wataalam wa Kata na Mitaa |

**2.2 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI**

Pamoja na changamoto zilizopo kwa wafugaji na wavuvi. Sekta hii imeimarishwa ili kuwaongezea nguvu ya kipato wafugaji hasa maeneo ya mijini, kutoa elimu kwa wavuvi kuondokana na uvuvi wakutegemea ziwa na badala yake kuanzisha ufugaji wa Samaki kwa kuchimba mabwawa ya kufugia samaki na kuondokana na kutegemea uvuvi wa ziwani pekee. Kwa muda unaotolewa taarifa mafanikio kadhaa yamefikiwa kama inavyoonesha katika jedwali hapa chini;

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 25 (e) | Kuanzisha mashamba darasa ya malisho katika kila Halmashauri ya Wilaya ili wafugaji wa asili wajifunze jinsi ya kuboresha na kuhifadhi malisho (feed banks) hususan wakati wa kiangazi na ukame. | Jumla ya wafugaji 933 wamefundishwa namna ya uanzishaji wa mashamba ya malisho. Aidha, Mashamba darasa ya malisho 6 yameanzishwa Katika kata za Kahama, Buswelu, Ilemela, Kiseke, Nyasaka na Kawekamo,<br><br>Mashamba darasa ya Malisho 4 yameanzishwa katika Kata za Ilemela, Kawekamo na Nyasaka |
| | Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya teknolojia ya uhamilishaji +B47:D5ili kuboresha koo safi za mifugo nchini kwa kutoa huduma za uhamilishaji kwa wafugaji kwa gharama nafuu kupitia ruzuku itakayowekwa katika mbegu za uhamilishaji. | Jumla ya wafugaji 195 kutoka kata za Ilemela, Kiseke, Kahama Nyamhongolo, Kawekamo, Kitangiri na Buswelu, Bugogwa wamepata huduma ya uhamilishaji kwa mifugo yao. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| | Kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji na vikundi juu ya ufugaji wenye tija | Taasisi ya Angeline Foundation kwa kushirikiana na Integrity Foundation na SUDAMA Investment ilifanikiwa kufundisha vikundi 5 vya Vijana na wanawake ufugaji wa sungura na kuku katika kata ya Kirumba 3 Shibula vikundi 2 |
| 25 (1) | Kuendelea kununua na kutoa **chanjo za magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya mifugo na binadamu na kuwezesha bias**hara ya mifugo katika soko lakimataifa, hususan Ugonjwa wa Homa ya Mapafuya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Bonde la Ufa (RVF) na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR). | Hakuna chanjo yoyote ya CBP-P,RVF na PPR iliyotolewa kwa ng'ombe na mbuzi, Ila jumla ya mbwa1450 walipatiwa chanjo ya kichaa, kuku 38,200 walichanjwa kideri, 25,000 gumboro.kutoja kata za Buswelu, Ilemela, Buzuruga, Kitangiri, Kawekamo, Pasiansi, Ibungilo,Nyakato, na Kirumba. |
| 26(c) | Ujenzi na uboreshaji wa mialo ya kisasa ya kupokelea mazao ya Uvuvi umetekelezwa katika Kanda ya Pwani ya Bahari ya Hindi (3), ziwa Tanganyika (4) na Ziwa Victoria (6). Aidha, Mialo 19 ya ukanda wa Ziwa Victoria imekarabatiwa | Kujenga mzani wa kupima magari ya mizigo yatokayo katika soko la kimataifa la Samaki Mwaloni Kirumba, Mzani wenye uwezo wa kupima uzito wa tani 80 za mizigo ya Samaki na mazao yake (Construction of Weigbride at Mwaloni Fish Market) Ofisi za mfumo wa kukatishia ushuru zimeshajengwa na kupauliwa kwa sasa tuko kwenye hatua za ukamailishaji (Finishing) vilevile Msingi (Foundation) umeshatengenzwa tayari kwa jili ya kuweka mzani (Installation) |
| | | Kurekebisha daraja la kupokelea mizigo ya mazao ya Uvuvi mwaloni kirumba (Repair of floating jetty), Vyuma vyote chakavu na vyenye kutu (plates) zimetolewa na kuwekwa vingine (repairing) na kupakwa rangi (painting) tayari kwa hatua ya kumwaga zege. |
| | | |
| 27(a) | Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya Msingi vya wavuvi wadogo wadogo kwa lengo la kuwakopesha vifaa vikiwemo zana za uvuvi katika maeneo ya mito kwa kupunguza kodi na kuviwezesha vikundi hivyo vikopesheke. | Kikundi 1 cha wavuvi wadogo wa Mwalo wa Mihama kimekopeshwa vifaa na zana bora za uvuvi vyenye thamani ya Tshs 80,000,000/= |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 27(k) | Kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa kuchimba mabwawa kwa lengo la kuongeza lishe bora pamoja na kuongeza ajira kwa vijana | ❖ Jumla ya mabwawa 47 katika Kata 6 za Sangabuye, Bugogwa, Kirumba, Kawekamo, Buswelu na Kahama yamechimbwa na samaki wamepandikizwa na wavuvi wadogo. |
| | Kutoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki 350 ya ufugaji bora wa samaki ifikapo Disemba 2017 | ❖ Wafugaji wa samaki 120 wamefundishwa mbinu za uvuvi na ufugaji wa samaki wa kisasa. |
| 27(i) | Kushirikiana na wadau wa ufugaji samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kujenga mabwawa ya kufugia samaki na kuongeza uzalishaji na kupanua wigo wa ajira kwa vijana. | Jumla ya mabwawa 44 ya kufugia samaki yamejengwa kati ya 66 kwa kipindi cha kuanzia 2015 - 2017 katika kata za Sangabuye, Bugogwa, Kirumba, Kawekamo, Buswelu, Kahama na Shibula. |
| 27(o) | Kuhamasisha uchimbaji wa mabwawa na ufugaji wa samaki katika maeneo yenye ukame kwa lengo la kuongeza lishe bora pamoja na kuongeza ajira kwa vijana. | Jumla ya mabwawa 15 yamechimbwa na kupandikizwa samaki katika kata za kirumba, Kawekamo, Buswelu na Kahama. |
| 27(p) | Kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija. | Kutokana na uchumi wa Ilemela kwa sehemu kubwa hutegemea uvuvi, mpaka sasa jumla ya doria 108 zimefanyika ili kuzuia uvuvi haramu, aidha elimu inaendelea kutolewa kwa wavuvi ili waondokane na uvuvi haramu. Wizara imeagiza zana bora zinazokubalika kwa uvuvi endelevu. |

## 2.3 VIWANDA NA BIASHARA

Katika kuitikia wito wa Mhe Rais wa awamu ya tano wa kuwa na Tanzania ya viwanda yenye mwelekeo wa kuwa na Uchumi wa kati, tumefanikiwa kubainisha maeneo mawili ya uwekezaji wa viwanda ambapo eneo la Nyamhongolo lenye ukubwa wa hekta 72.7 linaandaliwa Mpango kabambe na eneo la Ihalao lenye ukubwa wa ekari 650 yametengwa kwa ajili ya kanda Maalumu ya Kiuchumi. Maeneo haya yatamilikiwa na Halmashauri na hivyo kuwa chanzo cha kuiongezea kipato Halmashauri katika siku zijazo.

Vilevile, Jimbo kwa kushirikiana na sekta binafsi kuanzia Mwaka 2015 hadi Disemba, 2017 tumefanikiwa kuanzisha viwanda vipya 102 ikiwa Viwanda 7 ni vya kati na 95 ni vidogovidogo. Aidha, tunaendelea kutoa elimu na kuwahamsisha wananchi kushiriki katika Uchumi wa viwanda.

Tumefanikiwa pia kuhamasisha jamii na kuwaandaa wananchi kwa kutoa elimu ya namna bora yakuwa na uwekezaji wa viwanda wenye tija. Kupitia urafiki tulioujenga na Wafanyabiashara kutoka nchini Korea ya Kusini, makubaliano kadhaa yamefanyika kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Jiji la Deagu la nchini Korea.

Makubaliano yaliyofikiwa ni pamoja na:

1. Uanzishwaji wa Kiwanda cha nguo na kuanzisha mtaala maalumu katika Shule yetu ya Sekondari ya Wavulana ya Bwiru;

2. Kuanzisha kiwanda cha kuzalisha maji yatakayojulikana kama *Victoria Pure Drinking Water.*

3. Kuanzisha kitengo cha kufundisha wanafunzi matumizi ya mitambo mikubwa ya kutengeneza barabara katika chuo cha VETA kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi.

Uhamasishaji wa sekta binafsi kushiriki katika kujenga uchumi wa viwanda kwa kuingia ubia na wawekezaji kutoka nje ya nchi umefanyika. Vikao vya awali pamoja na wawekezaji toka Korea ya kusini vimefanyika Jimboni kupitia fursa zilizopo lakini pia kuona ni maeneo gani yanauhitaji mkubwa wa uwekezaji. Viongozi na watendaji kadhaa akiwemo Mstahiki Meya, Mbunge, Mkurugenzi wa Manispaa kwa nyakati tofauti wamepata fursa ya kusafiri kwenda Korea ya Kusini, ikiwa ni maandalizi ya kuwa na uwekezaji endelevu.

Katika hatua nyingine ya kuunga mkono sera ya Tanzania ya Viwanda, Kiwanda kipya cha kuzalisha maji yenye jina la “MWANZA Pure drinking water” kinachomilikiwa na wazawa cha FIDES Investment Ltd kimeanzishwa Kata ya Nyamhongolo nakutoa ajira kwa watanzania.



***Timu ya wawekezaji kutoka Korea ya kusini ilipofika kuriport katika ofisi ya mkuu wa mkoa. Waliokaa kutoka kushoto ni Naibu Mstahiki Meya Shaban Maganga, RAS Ndg Clodwing Tweve, Mbunge wa Jimbo Dkt A.S.L.Mabula, RC John Mongela, Mkuu wa msafala toka Korea Ndg Son, DC Ilemela Dkt Leonard Masale na Mkurugenzi wa Manispaa Ndg. Paul John Wanga, waliosimama baadhi yao ni Katibu wa Mbunge Ndg. Kheri D. James, Mkurugenzi wa Mwauwasa Eng. Anthony Sanga, Mkurugenzi wa Jiji Ndg Kiomoni Kibamba, na wadau wengineo wa maendeleo.***




***Timu ya wawekezaji toka Korea ya Kusini ilipata fursa ya kumtembelea ofisini kwake Mhe. Mwl. Kasimu Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kutoa zawadi ya jezi namba 5 ikiwa ni ishara ya kuunga mkono kauli mbiu ya Mhe. Dkt John Pombe Magufuli ya "HAPA KAZI TU".***



***Timu ya wadau wa maendeleo waliofika ofisi ya Mhe. Mwl. Kassimu Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutoka kushoto ni Ndugu Kaizer, Dkt. Mganga, David Mabula (Toka Taasisi ya VMPF) Mhe. Waziri Mkuu, Dr Angeline Mabula Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Mhe Shaaban Maganga Naibu Mstahiki Meya, na Eng Anthony Sanga Mkurugenzi wa MWAUWASA. Waliosimama kutoka kulia ni Amos K. Zephania Mchumi Manispaa ya llemela, William na Pamela Irengo mratibu wa KIcoT***

### 3.0 UWEKEZAJI

Mbunge wa Jimbo la Ilemela kwa kutambua dhamira ya Ilani ya uchaguzi katika suala zima la ajira na ukuzaji wa uchumi wa viwanda, ameamua kutumia fursa ya uwekezaji kama njia ya kutengeneza ajira, kukuza uchumi na kuboresha mazingira na muonekano wa mji. Katika kufanikisha azma hiyo, vikao kadhaa vya mazungumzo vimefanyika na baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje ambao wamekusudia kuwekeza katika Jimbo la Ilemela. Katika hatua zote za awali uongozi wa Mkoa na Wilaya ulishirikishwa. Aidha, mazungumzo na makubaliano yote ya awali yanasimamiwa na ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela. Maeneo yauwekezaji yaliyoainishwa na wawekezaji kwa kuzingatia mahitaji ya Jimbo ni pamoja na maeneo yafuatayo:

a) Uwekezaji kiwanda cha kuzalisha umeme wa jua (Solar Farm)

b) Ujenzi wa Hospital kubwa ya Saratani (specialized diagnostic Hospital)

c) Ujenzi wa kiwanda cha nguo

d) Ujenzi wa kiwanda cha maji ya kunywa

e) Ujenzi wa kiwanda cha kusindika Pilipili

f) Ujenzi wa karakana ya mitambo mikubwa

Miradi yote hii maadiko yake na makubaliano ya awali ya utekelezaji wa miradi hii yako Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua zaidi za utekelezaji.



***Katika picha, ni moja ya kikao cha awali kilichofanyika Nchini Korea ya Kusini 2016, kati ya Mbunge Dkt Angeline S.L. Mabula na baadhi ya wadau aliofuatana nao na Meya wa Jiji la Deagu Bw. Kwon Young-jin na wasaidizi wake.***



***Mhe. Mbunge Dkt. Angeline S.L.Mabula (Mb) katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa VETA Mama Hilderguard Bitegera pamoja na Ndugu Sima mwekezaji toka Korea akiwa na mwanae wakijadili suala la kuwezesha chuo cha VETA. Kuandaa wafanyakazi watakaoajiliwa katika Sekta ya Viwanda vya Nguo.***

**4.0 SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Hakuna ubishi kuwa raslimali pekee ambayo mwanadamu amepewa na Mwenyezi Mungu bila gharama yoyote ni ardhi. Changamoto kubwa tuliyonayo ni namna bora ya kuipanga, kuipima na kuiendeleza ardhi hiyo kwa kuipangia matumizi yaliyo sahihi na yenye kunufaisha watumiaji ardhi wa makundi yote. Serikali ina jukumu kubwa ya kutekeleza mipango yote ya uendelezaji ardhi, ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo utakao rahisisha umilikishaji wa ardhi na uhifadhi wa kumbukumbu muhimu ikiwemo michoro, na nyaraka mbalimbali za ardhi kwa kukamilisha ujenzi wa mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu zote za ardhi. Sambamba na hilo mpango wa matumizi bora ya ardhi nao umepewa kipaumbele, ukiwemo uandaaji wa mpango kabambe wa Miji Mikuu ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Aidha, utatuzi wa migogoro mbalimbali umekuwa ukifanyika katika maeneo mengi Jimboni.



***Ziara ya waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alipotembelea Wilaya ya Ilemela. Kutoka kushoto ni Mstahiki Meya Manispaa ya Ilemela Mhe Renatus B. Mulunga, Waziri wa Ardhi Mhe. Wiliam V. Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe John V. K. Mongela na Katibu wa Mbunge Comrade Kheri Denice James, kwa nyuma ni katibu wa waziri ndugu Hussein Sadick.***



***Katika picha ni baadhi ya wananchi wa Shibula wakiwa na Mbunge wao wakikagua mipaka ya eneo lenye mgogoro wa ardhi na mamlaka ya viwanja vya ndege.***



***Wakati mwingine ilibidi kupanda juu ya mlima ili kujiridhisha kwa kuona sehemu kubwa inayolalamikiwa na wananchi.***



***Afisa mipango miji Ndugu Kennedy Chigulu akitoa maelezo ya eneo lenye mgogoro kwa Mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L.Mabula (Mb)***



***Majadiliano juu ya jambo lililokuwa linaendelea katika mkutano wa hadhara Kata ya Kahama.***



***Mkurugenzi wa Manispaa Ndg John Paul Wanga akitoa ufafanuzi wa jambo katika moja ya mkutano ya Mbunge wa Jimbo la Ilemela.***



***Baadhi ya wananchi waliofurika katika mkutano wa Mbunge kutoa kero zao, Kata ya Kahama.***



***Moja ya wananchi waliofika kushukuru Mbunge mara baada ya kutatuliwa migogoro yao ya ardhi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Kahama.***

### 4.1 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA ARDHI

Pamoja na changamoto nyingi za migogoro ya ardhi, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango yake kwa ufanisi mkubwa. Moja ya mafanikio yanayotarajiwa kwa sasa ni kubadili mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi kutoka mfumo wa analogia na kuweka mfumo wa kidijitari. Ili kufanikisha azma ya Serikali ya kutekeleza Mipango ya kuendeleza na kuwa na makazi bora kwa wananchi wake. Ofisi ya Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Marafiki wa Korea ya Kusini tumetekeleza mambo yafuatayo;

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 37(a) (i) | Kujenga mfumo utakaorahisisha umilikishaji wa ardhi na kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa kukamilisha ujenzi wa mfumo unganishi wakuhifadhi kumbkumbu za ardhi (Intergrated Land Management Information System – ILMIS) | ❖ Pamoja na kuwa Mpango wa Wizara ni kuanza na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Ilemela kupitia marafiki wa Korea ya Kusini tayari tumebahatika kupata ruzuku ya dolla za Kimarekani 500,000 sawa na Fedha za kutanzania shilingi Bilion 1,115,000,000/= Zoezi la upigaji picha za anga iliwa ni maadalizi yakupata kumbukumbu sahihi zitakazo tumika katika kuunganishwa katika mfumo wa Wizara. Kazi ya upigaji picha tayari imefanyika na kinachoendelea kwa muda huu ni maandalizi ya kuanza rasmi kwa mradi wa kubadilisha taarifa za zilizopo kianalogia kwenda katika mfumo wa kidigitali<br><br>❖ Mfumo wa ukusanyaji kodi ya pango la ardhi *(Government e-payment Gateway System)* tayari umeunganishwa katika Halmashauri yetu.<br><br>❖ Mfumo wa kutunza kumbukumbu za Ardhi *(Management of Land Information System – MOLIS)* nakutoa mafunzo kwa watumishi wa idara husika umefanyika, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. |
| 37 (a) (iv) | Kuzijengea uwezo Halmashauri za miji na Wilaya kwa kuzipatia mafunzo na vitendea kazi, raslimali Fedha na wataalamu ili ziweze kupima viwanja na mashamba nchini | ❖ Vifaa vya kisasa vya kurahisisha upimaji viwanja vimenunuliwa, ambavyo ni Darubini za Kisasa za Upimaji wa Ardhi aina ya V90+ GPS-RTK.<br><br>❖ Mafunzo yamefanyika nje ya nchi ili kuwaandaa Watendaji kumudu matumizi ya mfumo mpya wa upimaji na utunzaji kumbu kumbu za ardhi. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 37(a) (viii) | Kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipango miji, Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Sheria zingine zinazohusiana na utawala wa ardhi. | ❖ Wananchi wamepata elimu kupitia mikutano ya hadhara iliyofanyika katika Kata za Kayenze, Sangabuye, Buswelu, Nyakato, Nyasaka, Mecco, Kawekamo, Ibungilo, Kirumba, Kitangiri, Pasiansi na Ilemela wakati wa mazoezi ya Urasimishaji Makazi. Pia elimu imetolewa kwa njia ya Redio, Television na Magazeti.<br><br>❖ Watendaji wa Kata 19, Watendaji wa Mitaa 52 na Wenyeviti wa Mitaa 165 wamepata elimu juu ya Sheria za Ardhi na Mipango Miji. |
| 37 (a) (ix) | Kuimarisha huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kuanzisha Mabaraza mapya ya Ardhi na Nyumba kwenye Wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi. | Jumla ya mabaraza ya Ardhi ya Kata katika Kata zote 19 yameanzishwa, kupewa elimu ya Sheria za Ardhi na yanaendelea kusikiliza na kutatua migogoro ya Ardhi. |
| 37(b)(iii) | Kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini. | ❖ Jumla ya viwanja 28,815 vimepimwa katika Kata mbalimbali za Manispaa, hususani katika maeneo yaliyofanyiwa Urasimishaji wa Makazi Holela.<br><br>❖ Halmashauri ya manispaa ya Ilemela inatumia mfumo wa Land Rent Managemnt System (LRIMS) na Government Electronic Payment Gateway (GEPG) kukadiria na kukusanya maduhuli ya Ardhi. |
| 37 (b) (iv) | Kuwapatia wananchi hati miliki pamoja na kusajili nyaraka nyingine za kisheria. | Jumla ya Hati miliki 6,508 za viwanja zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi |
| 37 (d) (i) | Kukamilisha uandaaji na uzinduzi wa Mpango Kabambe (Master Plann) wa Jiji | Mpango Kabambe Jiji la Mwanza ikiwemo na Manispaa ya Ilemela wa Mwaka 2015 hadi 2035 umekamilika, wakati wowote mpango huo utazinduliwa. Uzinduzi wake utafanyika taratibu zitakapokamilika. |
| 37 (d) (ii) | Kuhimiza ujenzi wa miji ya pembezoni (Satellite cities) katika miji yote ili kufanya miji hiyo ikue kwa kuzingatia Mipango Miji. | Miji ya Igombe na Kayenze imeandaliwa michoro ya Mipango Miji na hatua za upimaji zimeanza.<br><br>Upangaji wa wa Mji wa Kisasa wa Nyafura Satellite City umeanza kwa kufanya vikao vya uelimishaji na uhamasishaji kwa wananchi katika Mitaa 5 inayohusika katika Kata ya Sangabuye. |

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|---|
| 37 (d) (iv) | Kuendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya kurasimisha makazi yaliyopo katika maeneo ambayo hayajapimwa kwa lengo la kuyapanga na kuyapima viwanja na kutoa hati miliki za makazi | Kupitia zoezi la upimaji shirikishi jumla michoro 22 imeandaliwa katika maeneo yaliyofanyiwa urasimishaji na jumla ya viwanja vilivyopimwa 15,564 vimepimwa na wananchi 5,277 wamepatiwa hati zao. |

## 5.0 SEKTA YA UJENZI NA UCHUKUZI

Pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa na miundombinu ya Barabara, Madaraja, Vivuko n.k vinaboreshwa na kupitika wakati wote, kwa kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Jiji kwa ujumla wake tumebahatika kupata barabara ya njia nne baada ya Mhe Dr John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuamua kufuta sherehe za Uhuru kwa Mwaka 2016 nakuelekeza fedha za sherehe kutengeneza barabara hiyo yenye urefu wa km 5.2. Tunamshukuru sana kwa uamuzi huo wa busara. Mbali na barabara hiyo, Uwanja wa ndege wa Mwanza nao unapanuliwa uweze kuwa na hadhi ya kimataifa, wanufaika wakubwa ni wana Mwanza na kanda ya ziwa kwa ujumla zaidi sana ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela eneo ambapo uwanja huo upo.

### 5.1 VIWANJA VYA NDEGE

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 41(f) | ***Usafiri wa anga:*** Kukamilisha upanuzi wa kiwanja cha ndege hususani ni jengo la abiria na kufikia kiwango cha kimataifa. | Tayari upanuzi wa njia ya kurukia ndege umekamilika na ujenzi wa jumba la kurushia ndege unaendelea kwa kasi sana, Ujenzi wa kituo cha umeme, Ujenzi wa eneo la maegesho ya ndege pamoja na mizigo n.k |

### 5.2 UFUNGUZI WA BARABARA KALE

Kwa kutambua changamoto ya baadhi ya maeneo ndani ya Jimbo kuwa naugumu wa kufikika, Mbunge kwa kushirikiana na Katibu wa Mbunge na Waratibu wa Ofisi zake za kanda, aliendesha zoezi ya utambuzi na ufunguzi wa barabara za kale zilizopo katika maeneo hayo, kwa lengo kuunganisha maeneo mengine katika Jimbo ili kurahisisha mawasiliano ya wananchi. Barabara hizi zilikuwa zikitumika kipindi cha Mkoloni, na baadae zilitelekezwa na kuacha kutumika kiasi cha kufutika kabisa katika mtandao wa barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Barabara na maeneo yaliyonufaika na oparesheni fufua barabara kale yana jumla ya Km 27.5 ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi 58,217,000/= ikiwa ni Fedha kutoka “The Angeline foundation” shilingi 13,717,000/= na mfuko wa Jimbo shilingi 44,500,000/=. Barabara zilizofufuliwa ni;



***Kazi ya kufufua miundombinu ya barabara za kale ni muhimu kwa maendeleo ya Jimbo. Nawashukuru sana wananchi wa Sangabuye kwa kushiriki kikamilifu kufufua barabara za zamani***

1. Barabara ya Igogwe – Isanzu – Kabusungu - Igumamoyo - Nyafula hadi Sangabuye Km 9.3.
2. Barabara ya Kahama – Isela – Mwakalunde – Masemele – Ihalalo - Isesa – Ngwangwila hadi Iponyabugali Km 18.2.

Shukurani za pekee ziwandee *Katibu wa mbunge Comrade Kheri D.James,* Mratibu wa Jimbo ofisi ya Mbunge *ndugu Mpunji Mbegeje, Mhandisi wa Halmashauri Injinia Mussa Maloba* kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha dhamira ya Mbunge inatimia. Aidha, nimshukuru sana Mkurugenzi wa Manispaa *Ndg. John Paul Wanga* na menejimenti ya Manispaa ya Ilemela kwa ujumla wake kwa ushirikiano wao mkubwa katika kufanikisha kazi hii ya kuhakikisha maeneo yote ndani ya Jimbo yanafikika kwa urahisi.

***Wakati mwingine ilibidi kupasua miamba ili njia ipatikane. Hongera sana Katibu wa Mbunge Comrade Kheri D. James kwa usimamizi mzuri.***

***Harakati za kukarabati miundombinu ya barabara kata ya Kawekamo tukishirikiana na wananchi wa eneo husika.***

**5.3 PESA ZA MFUKO WA BARABARA**

Mara baada ya Uchaguzi Mkuu 2015, Jimbo la Ilemela lilikabiliwa na mvua kubwa zilizo athiri miundo mbinu ya barabara kwa kiasi kikubwa, hali ambayo ilimfanya Mbunge kuchukua maamuzi ya haraka kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Kamati ya Ulinzi na usalama ya Wilaya chini ya Mkuu wa Wilaya. Hatua zilizochukuliwa awali nikutembelea maeneo mbalimbali yaliyo athiriwa na mvua hizo, na baadae kupeleka maombi maalumu katika mfuko wa barabara ili kuomba Fedha za kunusuru miundo mbinu hiyo, Juhudi hizo zilizaa matunda. Mfuko wa barabara ulitoa Fedha kiasi cha shilingi milioni 600 ambazo kwa hakika zilisaidia kujenga na kuimalisha barabara katika maeneo hayo:-

- Barabara ya Lumala - Kiseke – Green view Km 2.5
- Barabara ya Kangaye - Makaburini Km 2.5
- Barabara ya Vuka - Kirumba mita 600
- Mtaro wa Villa Park – Safari lodge Mita
- Barabara ya CWT kwenda SDA Mita 700



***Katibu wa Mbunge Ndg Kheri D. James akikagua ujenzi wa moja ya barabara katika Kata ya Pasians***



***Ujenzi unaendelea vyema kuhakikisha miundombinu yote ya barabara inapitika wakati wote, katika Kata ya Kirumba Mtaa wa Kiyungi***




***Maandalizi ya ujenzi wa barabara ya lami toka Sabasaba – Kiseke – Buswelu Km 10.2 yameanza, jumla ya Tzs. Milioni 300 zimekwishalipwa kama fidia kati ya shilingi milioni 600 zinazotakiwa***



***Ujenzi wa barabara ya lami kuanzia Makongoro hadi Aoirport njia nne yenye Km 5.6 unaendelea kwa kasi kubwa***

## 5.4 UIMARISHAJI BARABARA ZA TANROAD NA HALMASHAURI

Jitihada zingine zimeendelea kufanyika kupitia TANROAD na Halmashauri kwa kuanza ujenzi wa barabara ya lami Km 18 kutoka Nyakato steel hadi Mhonze Tx na kutoka barabara kutoka Sabasaba hadi Buswelu Km 10.2. Lengo letu ni kuimarisha barabara zote kwa kuweka lami, kuziboresha "feederoad" na kuhakikisha maeneo yote yanafikika wakati wote na kuepusha msongamano katika barabara kubwa Mathalani Makongoro Road-Airport. Maeneo mengine katika utekelezaji yaliyotengenezwa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini;

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 39 (c) (i) | Kukamilisha ukarabati wa barabara zote unaoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami na changalawe katika Manispaa yetu. | ❖ Ujenzi wa barabara ya Makongoro Airport yenye Km 6.5 unaendelea vyema.<br>❖ Ujenzi wa barabara ya Sabasaba – Kiseke – Buswelu Km 10 hatua za kumpata mkandarasi zimekamilika na ujenzi utaanza Mwezi Machi 2018.<br>❖ Ujenzi wa barabara ya Nyakato Steel – Buswelu – Igombe TX yenye urefu wa Km 18 unaendelea. Mpaka sasa eneo la Km 1.2 limewekewa tabaka la lami na kazi inaendelea kwa kipindi cha Mwaka (2017/18).<br>❖ Kupitia maombi ya dharura ya 2017, kwa mara nyingine mfuko wa barabara umeidhinisha kiasi cha shilingi 690.0 milioni ili kutengeneza madaraja 6 zabuni imekwitangazwa ili kuwapata wakandarasi wa kutekeleza kazi hizo.<br>❖ Daraja la Nyakurunduma linalounganisha Kata ya Kawekamo na Ibungilo limetengenezwa.<br>❖ Daraja la (Msuka) Kilimahewa limetengenezwa na hivyo kuondoa adha ya mafuriko iliyokuwa inawakumba wakazi wa eneo hilo mara kwa mara na sasa shughuli mbalimbali za kibiashara zimeshamiri katika eneo hilo.<br>❖ Vivuko viwili vya waenda kwa miguu Mtaa wa Gedeli na mtaa wa Mecco vimetengenezwa kupitia Taasisi ya Mbunge. Jumla ya<br>shilingi 16,720,000/= zilitumika |

## 5.5 MADARAJA

Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja ili kuboresha hali ya barabara zote nchini. Kwa Halmashauri yetu ya Ilemela daraja la waenda kwa miguu eneo la Furahisha limekamilika na tayari linatumika. Tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuendelea kutuboreshea miundo mbinu yetu. Kukamilika kwa daraja hili kumebadili kabisa suru ya mji kiasi cha kuwa kivutio kwa kila anaepita eneo hilo. Aidha limekuwa likitumika pia na maharusi wetu kwa kupega picha.



***Daraja la Furahisha lililojengwa kwa Fedha za ndani kutimiza ahadi ya Mhe Dkt. John P.J.Magufuli. Picha ya chini inaonesha ujezi wa barabara ya Airport inayojengwa kwa Fedha zilizotokana na Mhe Rais kufuta sherehe za Uhuru Mwaka 2016. Kwaniaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela tunasema Asante sana Mhe Rais kwa uamuzi wa busara sana.***



***Daraja la Nyakurunduma linalounganisha Kata ya Kawekamo na Ibungilo likiwa limekamilika na kuondoa kero ya siku nyingi katika eneo hili.***



***Daraja la {Kwamsuka} kilimahewa, eneo ambalo lilikuwa korofi kwa kipindi kirefu na ambapo mfereji huu uliwahi kupoteza maisha kwa watoto wa Shule sasa limekamilika.***

## 5.6 VIVUKO

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | |
| 39 {h} {i} | Kuimarisha usafiri wa majini katika ziwa Victoria | Kuanza ujenzi wa kivuko kitakacho hudumia Kisiwa cha Base na Kata ya Kayenze. Tayari zabuni ya kazi hiyo imetangazwa jumla ya Fedha shilingi Bilioni mbili na milioni mia tatu (2,300,000,000/=) zimetengwa |

## 6.0 NISHATI

Serikali imeendelea kuboresha huduma za umeme kwa kusambaza umeme katika maeneo mengi Nchini. Halmashauri ya Manispaa yetu nayo ilibahatika kupata huduma hiyo katika maeneo ambayo awali hayakuwa na umeme



***Moja ya nyumba ambayo imepatiwa umeme katika Mtaa wa Chasubi Kata ya sangabuye na zoezi la uwekaji umeme wa REA unaendelea.***

## 6.1 Hali ya Umeme Wilayani.

Jimbo la Ilemela hupata umeme kutoka gridi ya Taifa kupitia njia ya umeme msongo kilovolti 220 kutokea Mkoani Shinyanga. Mahitaji mengine ya umeme katika eneo la jimbo ni jumla ya megawati 25. Umeme wa kawaida unapatikana vizuri kwenye maeneo yote yenye mtandao wa umeme. Mpaka sasa kuna mitaa 115 kati ya 171 imefikiwa na umeme. Hivyo mitaa 56 katika Wilaya haijafikiwa na huduma umeme.



***Baadhi ya nguzo ambazo zimesambazwa katika mtaa wa Chasubi Kata ya Sangabuye.***

## 7.0 MAWASILIANO

Kumekuwepo na changamoto ya mawasiliano katika baadhi ya maeneo Jimboni hususani maeneo yaliyoko pembezoni mwa mji. Kutokana na usikivu wa Serikali ya awamu ya tano tunategemea maeneo yote ndani ya Jimbo yatakuwa yamefikiwa kwa kuongezewa minara ya simu. Tayari Naibu Waziri mwenye dhamana ya Uchukuzi na Mawasiliano Injinia A. Nditiye ametembelea Jimboni akiambatana na Wataalamu wa Wizara pamoja na Wataalamu kutoka Halotel, ametuhakikishia kupatikana kwa huduma hiyo ndani ya kipindi kifupi kijacho.

## 8.0 HUDUMA YA AFYA

Kutokana na Sera ya nchi kuwa na Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata, ofisi yangu imeendelea kuhimiza jamii kuongeza kazi ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo yao. Nimeanzisha mradi wa tofali unaoratibiwa na Taasisi ya "The Angeline Foundation"utakaongeza kasi ya maendeleo, hivyo kuwataka wananchi kupitia Madiwani wao kujenga misingi, ofisi ya Mbunge itoe tofali, na Mkurugenzi wa Manispaa akamilishe ujenzi.

| IBARA | MAELEKEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50(a) (i) | Kuwa na zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila Kata, na hospital ya Wilaya kila Wilaya. | ❖ Agizo hili bado halijatekelezwa ipasavyo ingewaje hatua za makusudi zimeanza kuchukuliwa, Mfano, Mtaa wa Nyamwilolelwa, Nyamadoke tayari wameanza kunyanyua boma na mtaa wa Buganda tayari zahanati imekamilika na ilifunguliwa na Mbio za Mwenge Uhuru 2017.<br>❖ Hospitali ya Wilaya imeanza kujengwa na jengo la OPD limefikia asilimia 90 ya ukamilishwaji. |
| 50(a) (iii) | Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Afya kwa kupitia Sera ya Ubia na Sekta ya Umma | Hospitali inayomilikiwa na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA) imejengwa na iko katika hatua za ukamilishaji ili ianze kutoa huduma |
| 50(a) (ix) | Kujenga nyumba za watumishi karibu na vituo vyakutolea huduma | Nyumba moja ya Mtumishi imejengwa katika kituo cha afya Karume |
| 50 (l) | Kuunganisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji tarifa za afya ili kufikia lengo lakuwa mfumo mmoja unaokusanya na kutoa taarifa za afya nchini | Kupitia msaada wa computer 11 tulioupata kutoka TIGO tumeweza kupeleka computer hizo katika vituo vya afya 3, na zahanati 7 suala ambalo limerahisisha utekelezaji wa kuwa na mfumo unganishi unaotunza kumbukumbu zote za afya. |

Suala hili bado halijapokelewa vema kwani mwitikio bado ni mdogo. Aidha, Serikali imeongeza Bajeti ya Afya toka kiasi cha Tzs. 32 Bilioni Mwaka 2015/2016 hadi kufikia 275 Bilioni Mwaka 2017/18 na hivyo kuondoa upungufu wa madawa na vifaa tiba.

## 8.1 MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| *50 {i}* | Lengo la kila kijiji kuwa na Zahanati, Kata **kuwa na Kituo cha Afya na** Wilaya kuwa na Hospitali linaendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo huduma hizi hazijakamilika pamoja na kujenga hospitali za Wilaya katika Wilaya zote mpya. | Hadi sasa jumla ya Zahanati 4 zinaendelea kujengwa katika Kata ya Shibula, Nyamhongolo, Bezi. Aidha zahanati ya Buganda imekamilika na inatumika nyingine 2 zimetengewa bajeti ya Ujenzi katika Mtaa wa Nyamadoke Kata ya Nyamhongolo na Kisiwa cha Bezi Kata ya Kayenze,<br>Ujenzi wa hospitali ya Wilaya kwa jengo la dharura upo hatua za mwisho. Tumetenga Fedha za kuendelea na majengo mengine ya hospitali kwa Mwaka 2017/2018 |
| | | Ujenzi umefanyika katika kituo cha afya karume. Majengo yafuatayo yamejengwa, Jengo la upasuaji, nyumba ya watumishi, jengo la maabara, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la wodi ya wazazi. |
| **50 {iii}** | Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Afya kwa kupitia sera ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). | Wilaya ina jumla ya sekta binafsi 2 ambazo zipo hatua za mwisho kusaini miKataba ya utoaji wa huduma ya Afya. Aidha tunawadau wengine wanaoshirikiana na idara katika kutoa huduma za Afya |
| **50 {viii}** | Kutoa motisha kwa watumishi ambao wanafanyakazi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwajengea ushawishi wa kuendelea kutoa huduma za afya katika maeneo hayo. | Wastani wa Watumishi 237 hupewa motisha kwa kupewa posho na watumishi 17 wamepewa motisha kwa kupewa nyumba za kuishi katika vituo vyao vya kazi. |
| **50 {ix}** | Kujenga nyumba za watumishi karibu na vituo vya kutolea huduma. | Nyumba moja ya Matumishi imejengwa kituo cha Afya Karume. |
| | (b)Kuimarisha mapambano dhidi ya malaria kwa kufanya yafuatayo; | |
| 50 {b} {i} | (i)Kuwagawia wananchi vyandarua vyenye viuatilifu 306000 bila malipo. | Kuanzia Mwaka 2015 hadi Disemba 2017, jumla ya vyandarua vyenye viuatilifu 356,536 kati ya 361,760 zilizopangwa vimegawiwa kwa wananchi bila malipo. |
| 50 {b} {iv} | Kununua na kusambaza dawa za malaria katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya | Dawa za Malaria zimesambazwa katika vituo 16 Vya kutolea huduma za afya |

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 50 {c} | Kuimarisha upatikanaji wa huduma za dharura na za kawaida kwa wagonjwa kupitia vituo vya huduma za afya hapa nchini. Huduma hizi ni pamoja na magonjwa ya saratani, mishipa ya fahamu, mapafu, figo, huduma za magonjwa ya moyo, upasuaji mbalimbali ikiwamo upasuaji wa mifupa. | Kuanzia Mwaka 2015 hadi 2017, Jumla ya vituo 2 vinatoa huduma za dharura ( kimoja kwa ajili ya Saratani na kimoja kwa ajili ya upasuaji wa akina mama wajawazito) kwa mchanganuo ufuatao;<br>• Wagonjwa wa kawaida waliohudumiwa 342,820<br>• Huduma za dharura 134<br>• Saratani 15,368<br>• Upasuaji mbalimbali 201 |
| 50 { j} | Kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kuwa na Bima ya Afya ili kumudu gharama za matibabu. | Jumla ya wanaChama 560 kati ya 5000 waliotarajiwa wamesajiliwa TIKA na huduma zinaendelea kupatikana kwa kipindi cha 2016 hadi Desemba 2017. |
| 50 {n} | Kukarabati na kuimarisha huduma za kibinadamu katika vituo vya kutolea huduma za ustawi wa jamii vikiwemo makazi 17 ya wazee, mahabusu saba za watoto walio katika mkinzano na sheria pamoja na Shule moja ya maadilisho. | Vituo 16 vimetenga dirisha la kutolea huduma za wazee na kupewa vipaumbele pindi wafikapo kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya |
| | Halmashauri za Wilaya **zitaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kununulia vifaa vya kujimudu kwa lengo la kuwawezesha watu wenye ulemavu.** | Watu wenye Ulemavu wa ngozi 10 wametengewa jumla ya Tsh 1,100,000 kwa ajili ya kwenda KCMC kuchoma mionzi ya Ngozi kwa kipindi cha Mwaka 2015 |
| **50 {o}** | Kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za makundi maalumu wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi (albinism) na watoto wanaoishi mitaani ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Mtoto katika Halmashauri zote. | Jumla ya watu wenye ulemavu wa ngozi 115 Wamehudumiwa kwa kupewa mafuta ya ngozi kutoka Mwaka 2015 – hadi disemba 2017<br>(a) Jumla ya watoto 603 wamehudumiwa na kulindwa na Kamati za Ulinzi wa mtoto za vijiji<br>(b) Jumla ya kamati Mbili za Kata Shibula na Bugogwa na Kamati ya Manispaa ya ulinzi wa haki za watoto zimeundwa na kufanya vikao vyao vya ulinzi wa watoto. |
| | Kutoa huduma za mkoba (mobile clinic) hasa maeneo ya vijijini. | Jumla ya vituo 25 vimeimarishwa kwa ajili ya huduma ya mkoba (PENTA 3) na jumla ya watoto waliochanjwa 12455 ambayo ni 935 |

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Halmashauri zitahakikisha wazee wanatambuliwa na kupewa matibabu bure katika hospitali za Serikali. | Jumla ya wazee 9867 (katika Kata 19 wametambuliwa na wanapata matibabu bure<br><br>Zahanati na vituo vya Afya 16 zina madirisha ya wazee wanaotibiwa bure |
| | | Kuna Zahanati na Vituo vya afya zote 16 zina madirisha ya wazee wanaotibiwa bure |
| 50 {q} {i} | Kuzijengea uwezo Hospitali na Vituo vya Afya ili kutoa huduma kamili ya Afya ya Uzazi na Mtoto pamoja na upasuaji kwa mama wajawazito | Jumla ya vituo 25 vinatoa huduma ya mama na mtoto na kituo 12 zimejengewa majengo ya upasuaji, (3) Buzuruga, Kirumba na Ilemela vipo kwenye mpango wa ujenzi. Kituo cha Afya karume ujenzi umekamilika |
| 50 {q} {v} | Kuendelea kutekeleza mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMCTC) | Kiwango cha maambukizi kimepungua hadi kimefikia asilimia 1.6% toka 2.5 kwa Mwaka 2015<br><br>Jumla ya wajawazito 3195 wamepimwa maambukizi ya VVU katika vituo vya kutolea huduma ya afya kati yao 120 Waligundulika kuwa na VVU Disemba 2015 – Disemba, 2015 – Disemba 2017<br><br>Elimu ya kinga ya maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI ilitolewa katika Mitaa 120 |

### 8.2 UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA

Wilaya imefanikiwa kuanzisha ujenzi wa Hopitali ya Wilaya ambayo mpaka sasa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje limefikia asilimia 90 ya ujenzi. Mpaka sasa jumla ya **Tshs 572,299,039**.00 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa na Serikali Kuu zimetumika. Ili kukamilisha ujenzi wa awali wa Hospitali hii jumla ya Tshs **Tshs. 4,327,552,180** zinahitajika kujenga miundombinu ifuatayo;

| S/ NA | KAZI INAYOTAKIWA KUFANYIKA | GHARAMA TSHS. |
|---|---|---|
| 1 | Wodi ya Wanawake | 480,637,500.00 |
| 2 | Wodi ya wanaume | 480,637,500.00 |
| 3 | Wodio ya watoto | 470,637,500.00 |
| 4 | Jengo la Mionzi | 492,557,600.00 |
| 5 | Jengo la kufulia na Jiko | 182,550,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Jengo la kutakasia vifaa | 410,780,000.00 |
| 7 | Jengo la upasuaji | 641,579,680.00 |
| 8 | Jengo la kuhifadhia maiti | 184,800,000.00 |
| 9 | Jengo la wajawazito | 535,270,000.00 |
| 10 | Jengo la maabara | 448,102,400.00 |
| | **JUMLA** | **4,327,552,180.00** |

### 8.3 UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA AFYA KARUME

Serikali kuu imetoa kiasi cha **Tshs 500,000,000** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kituo cha Afya Karume kilichoko Kata ya Bugogwa. Utekelezaji wa ujenzi tayari umekamilika na majengo yafuatayo yamejengwa-Jengo la Upasuaji, Jengo la kujifungulia wajawazito, Nyumba ya Mtumishi, Jengo la maabara na Jengo la Kuhifadhia maiti, majengo haya yote yamekamilika.

Vilevile uongozi wa ngazi ya Wizara akiwemo Waziri wa Afya, maendeleo ya jamii,Jinsia wazee na Watoto, Katibu Mkuu wa Wizara wametembelea eneo la mradi na kuridhika na viwango vya ujenzi wa miundombinu ifuatayo;

Serikali pia imeidhinisha kiasi cha **Tsh 220,000,000/=** ikiwa ni gharama za ununuzi wa vifaa tiba, vifaa vya hospitali na vitendanishi kwa ajili ya kituo cha Afya karume. Fedha hizo zimepelekwa moja kwa moja MSD ambaye ndiye ataleta vifaa hivyo. Hadi sasa kituo kimepokea vifaa vyenye thamani ya **Tsh 48,981,300** ambavyo baadhi vimeingia kwenye majengo yaliyokamilika na vingine vinangojea ukamilishaji wa majengo



***Jengo la Upasuaji katika kituo cha afya Karume likiwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji***

**8.4 UPATIKANAJI WA DAWA MUHIMU**

Upatikanaji wa Dawa muhimu katika Vituo vya kutolea huduma za Afya vya Serikali umeongezeka kutoka 80% Mwaka 2015 hadi 93% Mwaka 2017. Kama nilivyobainisha hapo juu.



***Nyumba ya mtumishi iliyojengwa katika kituo cha afya Karume***

**8.5 MATUKIO YA KIJAMII**

Katika kipindi cha miaka miwili nimeshirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutoa misaada ya hali na mali katika nyaja zote za kijamii kama zinavyoonekana katika picha zifuatazo:




***Katibu wa Mbunge Comrade Kheri Denice James akiwa na Mkurugenzi wa Nitete Foundation ndugu Flora Lauwo wakikabidhi mashuka yaliyotolewa na "The Angeline Foundation" kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo, Dkt Angeline Mabula.***



***Kukabidhi mashuka na kuanza kutumika katika wodi ya watoto, waliosimama ni Afisa Tarafa Ndugu James Chuwa, Comrade Kheri Denise James Katibu wa Mbunge na muuguzi aliyekuwa zamu katika Zahanati ya Kata ya Kahama***




***Tunamshukuru sana Mhe Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia Ambulance moja katika kituo***

***cha Sangabuye, lengo ikiwa ni kuokoa maisha ya Mama mjamzito na mtoto. Kwa niaba ya wana Ilemela nasema asante sana Jimbo la Ilemela lilikuwa miongoni mwa Wilaya 100 za mwanzo zilizopata Gari la wagonjwa (Ambulance***





***Moja ya vyoo kumi vya kisasa vilivyofadhiliwa na benki ya dunia kupitia mamlaka ya maji safi na taka MWAUWASA kilichojengwa katika baadhi ya Shule za Msingi jimboni ikiwemo Shule ya Msingi Kitangiri A na B***




***Moja ya jengo la vyoo vya kisasa kabisa lililojengwa kwa msaada wa LVEMP wa kuboresha mazingira. Tulbahatika kujengewa vyoo hivyo katika Shule za Msingi 3 (Nyambiti, Nyasaka na Isenga)***



***Ujenzi wa Zahanati ya Nyamadoke katika Kata ya Nyamhongolo unaendelea ukiwa katika hatua za boma, Msingi umejengwa kwa nguvu za wananchi na mchango wa Mbunge tofali 2000 ambazo zimenyanyua boma hilo hadi kufikia hatua hiyo.***



***Jengo la zahanati ya Buganda Kata ya Shibula ambalo lilifunguliwa na mbio za mwenge Mwaka 2017, tayari huduma ya tiba inatolewa hapo.***




***Kompyuta 11 zilizotolewa na kampuni ya TIGO ikiwa ni msaada kwaajili yakuboresha utendaji kazi katika vituo vya afya na zahanati Jimboni. Vituo vyote vitatu vilipata computer moja moja pamoja na zahanati 8***

## 9.0 ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Jimbo la Ilemela lina jumla ya Shule 114 za Msingi kati ya hizo 40 ni za binafsi na Shule 74 ni za Serikali. Shule za Sekondari ni 46 kati yake Shule 24 za Serikali na Shule 22 ni za binafsi. Katika jitihada za kukabilina na changamoto mbalimbali za sekta ya elimu, kwa kipindi cha 2015 – 2017, nguvu kubwa tulielekeza katika kushirikisha wadau kwa kufanya harambee kubwa kwa kushirikiana na Halmashauri kukusanya Fedha na vifaa kwa ajili ya ununuzi wa madawati na ujenzi wa vyumba vya madarasa. Harambee hii ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Jimbo la Ilemela, Mgeni rasmi alikuwa Mhe. ASHATU KIJAJI Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango. Kupitia harambee hii wadau walimuunga mkono Mbunge kwa kuchangia Fedha na vifaa mbalimbali vya ujenzi ambavyo kwa hakika vimesaidia sana kupunguza changamoto katika Shule zetu.

Fedha zote zilizo kusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali zilisaidia kupata madawati 1,650 na ujenzi wa vyumba vya madarasa. Vifaa na madawati vyote vilikabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya na baadaye Mkurugenzi wa Manispaa alisambaza kwenye Shule mbalimbali. Aidha tulifanikiwa kugawa vitabu vya sayansi 720 vilivyogharimu shilingi 8,200,000/= katika shule za Sekondari Mihama, Ibinza na Kilimani zilizokuwa zimefanya vibaya katika mtihani wa taifa mwaka 2016.

Aidha, kutokana na Mpango wa Serikali ya awamu ya tano ya kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha nne, hatua hii imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaondikishwa katika Shule za Msingi na Sekondari kama ifuatavyo;

## 9.1 Shule za Msingi

(i) **Uandikishaji Darasa la awali**

Jimbo limeendelea na zoezi la uandikishaji wa watoto wa darasa la awali ambapo hadi kuishia Desemba 2017 imeweza kuandikisha kwa asilimia 94. Aidha, Wilaya kuanzia Mwaka 2015 hadi 2017, imefanikiwa kuvuka malengo ya uandikishaji kwa kila Mwaka kama ilivyooneshwa Katika **jedwali lifuatalo**;

***Jedwali: Uandikishaji Darasa la Awali Mwaka 2015-2017***

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wasichana | wavulana | Jumla | (%) |
| 2015 | 7382 | 4028 | 3832 | 7860 | 107 |
| 2016 | 7837 | 4571 | 4504 | 9075 | 169 |
| 2017 | 7667 | 4359 | 4291 | 8650 | 113 |

**(ii) Uandikishaji Darasa la Kwanza**

Jimbo kuanzia Mwaka 2015 hadi 2017 tumeweza kuandikisha kwa zaidi ya asilimia 106 ya lengo kama ilivyooneshwa katika jedwali lifuatalo;

***Jedwali: Uandikishaji Darasa la Kwanza Mwaka 2015-2017***

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wasichana | wavulana | Jumla | (%) |
| 2015 | 7,950 | 4595 | 4396 | 8,991 | 112 |
| 2016 | 9,168 | 7598 | 7286 | 14,884 | 162 |
| 2017 | 11,716 | 6185 | 5953 | 12,138 | 103 |

**(iii) Ujenzi wa Vyumba vya madarasa na Utengenezaji wa Meza na viti.**

Wilaya imeendelea kukamilisha utengenezaji wa madawati ambapo jumla ya madawati 9,007 kwa Shule za Msingi yametengenezwa na kukarabatiwa katika Shule mbalimbali. Hatua hii imepunguza upungufu wa madawati uliokuwepo kutoka madawati 13,346 (sawa na 52% ya mahitaji) hadi 4, 339 (sawa na 17% ya mahitaji). Mahitaji halisi ya madawati yalikuwa ni 25,825 Shule zote za Msingi za Serikali. Utengenezaji wa madawati kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali ili kumaliza upungufu unaendelea.

Vilevile tumekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 22 na kukamilika na vyumba 6 ukamilishaji unaendelea. Aidha, tumefanikiwa kujenga matundu ya vyoo 389 kati ya matundu 2,924 yanayohitajika hadi kufikia mwezi Desemba 2017 katika Shule za Msingi ili kukabiliana na upungufu.

Ili kuhakikisha mdondoko unapungua kwa wanafunzi wa Elimu Msingi unapungua kutoka wastani wa asilimia 1 hadi 0 kufikia Disemba 2017, Halmashauri kwa kuimarisha usimamizi na ufuatailiaji imeweza kupunguza mdondoko wa wanafunzi katika Elimu Msingi umepungua kutoka asilimia 1hadi kufikia asilimia 0.3 Ili kuwandaa vema watoto wanaotarajiwa kujiunga na darasa la kwanza, Halmashauri ilipanga kuanzisha madarasa ya Elimu ya Awali katika Shule zote za Msingi 74 ifikapo Disemba 2017. Utekelezajiwa suala hili ni kwamba madarasa ya Elimu ya Awali 74 yameanzishwa katika Shule zote za Msingi 74

(iv) **Mapokezi ya Fedha ya Ruzuku malipo**

Kufautia mpango wa Elimu bila Malipo, Serikali kuanzia mwezi Desemba 2015 hadi Desemba 2017 imeendelea kutoa Fedha ya ruzuku katika Shule zote 74 za Msingi Jimboni. Hadi sasa kiasi cha Tzs. 750,868,340/= zilizotolewa kama inavyoonekana katika jedwali;

***Jedwali la Mapokezi ya Fedha ya Ruzuku malipo***

| Na | Mwaka | Lengo | Mapokezi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2016 | 275,340,000.00 | 275,340,000.00 | 100 |
| 2 | 2017 | 475,528,340.00 | 475,528,340.00 | 100 |
| **Jumla** | | **750,868,340.00** | **750,868,340.00** | **100** |

Kila jambo jema halikosi changamoto. Sera ya elimu bila malipo ilileta ongezeko kubwa la uhaba wa vyumba vya madarasa, jambo ambalo ilinilazimu kubuni mradi wa ufyatuaji tofali uliofadhiliwa na Shirika la Nyumba la Taifa NHC. Mradi huu umekuwa ni chachu ya kumaliza kero za miundombinu katika Shule zetu. *Tayari maboma 22 ya vyumba vya madarasa yamejengwa kwa mfumo shirikishi yaani Jamii inajenga msingi, Mbunge anatoa matofali na Mkurugenzi anakamilisha ujenzi.* Mradi huu umeendelea kuchangia shughuli za maendeleo jimboni na umeleta ajira kwa vijana na wanawake wapatao 12

## 9.2 Elimu Sekondari

(i) **Uandikishaji wa Kidato cha Kwanza**

Katika kipindi cha 2016 – 2017 wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ni 11,175 kati yao wasichana ni 5,513 na wavulana ni 5,662. Aidha, undikishaji umekuwa ukiongezeka Mwaka hadi Mwaka kama ilivyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo;

***Jedwali la Uandikishaji Kidato cha Kwanza Mwaka 2015-2017***

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wasichana | wavulana | Jumla | |
| 2015 | 6324 | 2914 | 2705 | 5619 | 88 |
| 2016 | 6239 | 2748 | 2622 | 5370 | 86 |
| 2017 | 6243 | 2765 | 3040 | 5807 | 92 |
| 2018 | 9105 | 3581 | 3745 | 7326 | 80 |

(ii) ***Ujenzi wa vyumba vya madarasa na utengenezaji wa viti na meza***

Jimbo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limeendelea kukamilisha utengenezaji wa madawati ambapo jumla ya seti 900 (seti za meza na viti) na kukarabati meza/viti 1298 kwa Shule za Sekondari zimetengenezwa na kugawiwa katika Shule mbalimbali. Vilivile, ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa Shule ya Sekondari Mnarani na Kiloleli umefanyika. Aidha, Ujenzi wa vyumba viwili na ukarabati vyumba 10 vya madarasa chini ya programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP II) umekamilika na madarasa yanatumika katika Shule ya Sekondari Sangabuye.

(iii) ***Ukarabati wa Shule ya Sekondari Bwiru wavulana***

Shule ya Sekondari ya Ufundi Bwiru Wavulana ilipokea Fedha kiasi cha Tshs. 825,841,642.00 toka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Fedha hizi ni kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Shule kongwe katika majengo ya Shule yakiwemo madarasa 19, mabweni 11, jengo la utawala 01, maabara 02, maktaba 01, vyoo 09, mfumo wa maji, mfumo wa umeme, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA), Bwalo la chakula na jiko. Shughuli hii ya ukarabati imekamilika kwa 98% na hivi sasa kazi iliyobaki ni kumalizia ukarabati wa jiko.

(iv) ***Mapokezi ya Fedha ya Ruzuku Elimu bila malipo***

Katika jimbo la Ilemela tulifanikiwa kupokea toka Serikali Kuu Fedha kwa ajili ya elimu bila malipo kiasi cha jumla ya Tshs. 3,428,819,376 kuanzia Mwaka 2015 hadi Desemba 2017. Aidha, tunaishukuru Serikali kwa kuwezesha mazingira mazuri kwa wanafunzi katika Shule za Sekondari. Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

***Jedwali la Mapokezi ya Fedha ya Ruzuku malipo***

| **Na** | **Mwaka** | **Mapokezi** |
|---|---|---|
| 1 | 2015 | 129,786,000.00 |
| 2 | 2016 | 1,634,868,000.00 |
| 3 | 2017 | 1,664,165,376.00 |
| **JUMLA** | | **3,428,819,376.00** |

**PICHA ZENYE KUONESHA WADAU MBALIMBALI WALIOUNGA MKONO JITIHADA ZA MBUNGE**




***Meneja wa LAPF tawi la mwanza Ndugu Yesaya Mwakifulefule akikabidhi mifuko 225 kwa Mbunge wa Jimbo***




***Mkurugenzi wa Mwanza Huduma Ltd Ndugu Zulfikari akikabidhi mifuko 200 ya saruji kuunga mkono juhudi za Mbunge za kupunguza kero ya miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari Jimboni.***



***Ndugu Gerald Yusuph akikabidhi mifuko 300 ya sementi ikiwa ni mchango wa wadau wa Mwanza Cosmopolitan ambao hawakuwa nyuma kuhakikisha adhma ya kumaliza kero ya madarasa inakamilika.***




***Mgeni rasmi katika harambee yakuchangia Fedha kwa ajili ya uboreshaji miundo mbinu ya elimu Dkt Ashatu Kijaji, Naibu waziri wa Fedha na mipango alichangia shilingi 15,000,000/=,***



***Kulia ni Meya wa Manispaa ya Ilemela Mstahiki Renatus Mulunga, Dkt Angeline Mabula Mbunge wa Jimbo, Mhe John Mongela Mkuu wa mkoa wa Mwanza, Dkt Leonard Masare Mkuu wa Wilaya ya ilemela na Ndugu John Paul Wanga Mkurugenzi wa Manispaa wakisikiliza hotuba ya Naibu waziri Kijaji.***



*Baadhi ya waBunge na viongozi wa Chama na Serikali walioshiriki kuunga mkono juhudi za Mbunge wa Ilemela katika harambee iliyoandaliwa kwa ajili yakuchangia Fedha kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu ya elimu. Kutoka kushoto ni Mhe Stanslaus Mabula (Mb), Mhe Stanslaus Nyongu (Mb), Mhe Jumanne Kishimba (Mb), Ndugu Israel Mtambalike (MNEC),Ndugu Jacob Shibiliti (MNEC) na Mhe Manju Msambya mkuu wa Wilaya ya Ilemela mstaafu.*




*Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan akibabidhi moja ya madawati 537 yaliyotolewa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania . Pichani ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilemela Nelson Mesha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Ndg John Paul Wanga na Mstahiki meya wa Manispaa ya Ilemela Mhe Renatus Mulunga. Kwa pembeni anaonekana Mwenyekiti wa CCM Mkoa Dkt Anthony M. Dialo na Naibu meya Mhe Shaban Maganga.*




***Picha ya chini na juu ni sehemu ya madawati yaliyotolewa na taasisi ya "The Angeline Foundation" kwenye shule za msingi jimboni***





***Katika Picha ni baadhi ya viongozi RC, DC, Mbunge, Meneja Azania Banki na wanafunzi wakishuhudia madawati 100 yaliyotolewa na Azania banki, dawati 50 jimbo la Ilemela na dawati 50 jimbo la Nyamagana.***



***Kiongozi wa Bodaboda wilwya ya Ilemela wakikabidhi madawati 30 ikiwa ni mchango wao kuunga juhudi za Mbunge kupunguza kero ya madawati jimboni, na walipokea cheti cha shukurani kwa mchango wao***





***Picha mbili hapo juu ni mapokezi ya vitabu na computer toka Taasisi ya BRACK kwa ajili ya Shule za msingi***



***Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan akipanda mti wa kumbukumbu siku ya uzinduzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela 23.11.2016***

## 10. MAJI

Utekelezaji wa Miradi yamaji toka Desemba 2015 hadi Disemba 2017 Jimbo la Ilemela katika Mkoa wa Mwanza ni moja ya wanufaika wakubwa wa mradi wa maji safi na usafi wa mazingira unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) ambao utekelezaji wake unayofadhiliwa na Serikali ya Tanzania pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank, EIB), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Francaise de Development, AFD) kwa gharama ya ***Euro Milioni 104.5.*** Tayari wakandarasi walishapatikana tangu tarehe 16/2/2017 na wako katika maeneo ya kazi baada ya kutia saini mikataba yao, utekelezaji wa kazi za Ujenzi wa Mradi zilianza rasmi tarehe 22 Mei 2017. Kwa Miradi inayotekelezwa ndani ya Jimbo la Ilemela wetu wana Ilemela Mkataba ulisainiwa katika eneo la Nyasaka mahali ambapo tanki la maji linajengwa, mradi huo utagharimu kiasi cha ***Euro 14,689,448.35.*** Kampuni za M/S. JOS. HANSEN & SOEHNE GmbH in JV with M/s. JR INTERNATIONAL BAU GmbH kutoka Ujerumani ndiyo zinazotekeleza mradi huo.

Kazi zinazofanyika kupitia mradi huu ni kama zifuatazo:-

a) Kuboresha huduma ya majisafi katika maeneo ya milimani hususani maeneo ya Ilemela ni *Nyasaka, na Kitangiri* (Bugarika, Nyegezi, Capripoint, *Mjimwema,* Nyakabungo upande wa Nyamagana) ambayo hayapati maji vizuri kwa sasa. Wanufaika wa mradi wanakadiriwa kuwa wananchi 105,649 (kwa makadirio ya Mwaka 2025).

b) Shughuli za mradi ni pamoja na utandazaji wa mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji za vipenyo kati ya 315mm na 50mm zenye urefu mita 64,820. Jumla ya wateja 20,000 watanufaika na mradi huu. Uwezo wa tanki zitakazojengwa ni maeneo *ya Kitangiri (lita 500,000), Nyasaka (lita 1,000,000),* Mjimwema/Nyakabungo (lita 1,200,000), Nyegezi (lita 1,200,000), na Bugarika (mawili ya lita 800,000 na 200,000).

c) Kubadilisha mabomba ya zamani yaliyochakaa na kuongeza mtandao wa mabomba. Kazi hii inahusu maeneo ya *Makongoro na Nyakato* (Jumla ya urefu wa mabomba mita 15,770. Aidha, mtandao wa mabomba utaongezwa kwa jumla ya mita 2,000 eneo la Makongoro.

d) Kubadilisha viungio katika mtandao wa majisafi - “Valves and Fire hydrants” kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kusambaza maji na kuongeza wigo wa kitengo cha zimamoto kukabiliana na majanga ya moto pindi yakitokea. Hivyo jumla ya “Fire hydrafts” 22 zitawekwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu.

**Utekelezaji wa Mradi hadi 31 Desemba 2017.**

Hadi kufikia Desemba 2017, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni kama ilivyoainishwa katika majedwali yafuatayo:

**Mradi wa visima 10 vinavyotekelezwa Jimboni**

Pamoja na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji, kama inavyoonesha hapo juu, tunayo pia miradi iliyokuwa inafahamika kama miradi ya vijiji kumi (10) inayotekelezwa katika maeneo ya *Kayenze, Sangabuye, Nyafula, Igogwe, Kabusungu, Nyamwilolelwa, Kahama na Nyamadoke*, ambayo ilianza kutekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi huu uko chini ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji *(Water Sector Development Programm WSDP)* kupitia Programu ya kitaifa ya usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini ‘NRWSSP – National Rural Water Supply and Sanitation Programm’. Aidha utekelezaji wa mradi huu umekuwa wa ukisuasua ingawaje hatua iliyofikiwa sasa inaridhisha kwani umefikia 70%.

**Gharama za mradi na pesa zilizotumika mpaka sasa ni kama ifuatavyo:**

| Eneo la mradi wa Maji | Bajeti | Matumizi | Pesa iliyopo | % ya utekelezaji | Idadi ya wanufaika |
|---|---|---|---|---|---|
| Sangabuye | 697,589,398.00 | 553,824,056.40 | 143,765,342.00 | 90 | 7535 |
| Igogwe, Nyafula na Kabusungu | 1,012,342,500.00 | 362,636,500.00 | 649,706,000.00 | 65 | 17,750 |
| Kahama -Nyamadoke | 1,134,603,085.70 | 408,522,450.10 | 726,080,636.00 | 50 | 11,867 |
| Chanzo cha Maji Igombe | 2,158,024,000.00 | 769,259,000.00 | 1,388,765,000.00 | 40 | 0 |
| Nyamilolelwa | 1,038,005,100.00 | 554,884,320.00 | 483,120,780.00 | 75 | 12,056 |
| Kayenze | 618,704,554.65 | 618,704,554.65 | 0 | 100 | 9,865 |
| **Jumla** | **6,659,268,638.00** | **3,267,830,881.15** | **3,391,437,757.00** | **wastani 70** | **59,073** |



***Tanki la maji lililojengwa Kata ya Kahama ambalo liliwekewa jiwe la Msingi katika mbio za mwenge za Mwaka 2017***



***Mradi mkubwa wa maji unaofadhiliwa na shirika na Maendeleo la Ufarasa wenye thamani ya Euro Milion 104.2 unaendelea kujenga katika vilima vya kata ya Nyasaka. Picha ya chini inaonesha kazi ya kutandaza mabomba inaendelea, mradi unasimiwa na MWAUWASA***





*Sehemu ya Mabomba vitakavyotumika kusambaza maji katika vituo vya kuchotea maji katika mtaa wa Kilabela Kata ya Kahama.*

| IBARA | MAELEZO YA ILANI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 54 (a) | **Maji safi;** Kuboresha huduma za maji kutoka asilimia 67.7 Mwaka 2015 hadi asilimia 85 Mwaka 2020. | Jumla ya miradi 8 ya maji katika maeneo ya *Kayenze, Sangabuye, Nyafula, Igogwe, Kabusungu, Nyamwilolelwa, Kahama na Nyamadoke* iko katika hatua mbali mbali za utekelezaji, mradi mmoja wa Kayenze umekamilika na unatumika kama ifuatavyo:<br>• **Mradi wa maji Kayenze;** Ujenzi umekamilika na kukabidhiwa kwenye Jumuiya ya watumiaji maji. Jumla ya vituo 13 vyakuchotea maji vimejengwa, Nyumba ya mitambo na ufungaji wa mitambo pamoja na mtandao wa mabomba, ulikamilika Mwaka 2016.<br>• **Mradi wa Kusambaza maji Sangabuye** :Utekelezaji wake umefikia 90% ukihusisha Ujenzi wa tanki la 135$m^3$, Vituo vya kuchotea maji 14, Ujenzi wa nyumba ya mitambo na ufungaji wa mitambo na mtandao wa mabomba ya kusambazia maji. Ufungaji wa pampu ya maji (booster pump), ufungaji wa control panel, pamoja na ufungaji wa jenereta umekamilika. Mkandarasi kwasasa anafanya majaribio ya kusukuma maji, tunatarajia mwezi wa pili mradi uanze kutumika.<br>• **Mradi wa maji Igombe**: Ujenzi wa chanzo cha maji, Ujenzi wa tenki la kupokelea maji (Sump well), Ujenzi wa tenki la maji la maji Igombe la 225m3, Ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji (pump house) na uwekaji mitambo na ulazaji wa mabomba ya kupeleka maji kwenye tanki la Igombe na Igogwe ambacho kitahudumia miradi ya *Nyafula, Igogwe, Kabusungu, Nyamwilolelwa, Kahama na Nyamadoke.*<br>• **Mradi wa Maji Kahama na Nyamadoke:** Ujenzi wa tenki la maji la 225m3 Ujenzi wa vituo 22 vya kuchotea maji ambavyo vyote vimeshajengwa, Ujenzi wa manywesheo ya mifugo 2/3, yameshajengwa, Ujenzi wa nyumba ya mitambo ya kusukuma (booster house) na tenki dogo la kupokelea maji (Sump well), Ujenzi wa mtandao wa mabomba wenye urefu wa 28km.<br>• **Mradi wa Maji Nyamwilolelwa** Ujenzi wa vituo vya kuchotea 16/20 vimekishajengwa, Ujenzi wa mfumo wa kuvunia maji ya mvua ambapo matenki madogo 2 ufungaji wa kinga maji (gatters) katika Shule ya Msingi ya Umoja, Mhonze na Nyamwilolelwa, Ujenzi mtandao wa mabomba wenye urefu wa 7/17km zimefika site.<br>• **Mradi wa Maji Nyafula, Igogwe na Kabusungu** vituo 33 vya kuchotea maji tayari vimeshajengwa, Ujenzi wa tanki la maji la 225m3 ambalo limekamilika kwa 95%, Ujenzi wa mtandao wa mabomba wenye urefu wa 38km haujaanza unasubiri kukamilika kwa kwa mapitio ya usanifu wa mabomba. |

| | | |
|---|---|---|
| 54 (c) | Kukamilisha miradi mikubwa ya maji na kuhakikisha vijiji au mitaa yote inapata maji | Jumla ya mitaa 39 itanufaika baada ya miradi yote kukamilika kama ifuatavyo; Sangabuye; Mtaa wa Nyashimba, Isesa, Igumamoyo Ng'wangila, Ihalalo, Imalang'ombe, Lwashi, Nyamiswi<br><br>Kabusungu, Nyafla, Igalagala Kata yaa Kayenze; Lutongo, Iponyabugali, Iseni. Kahama; Isela, Kadinda, Magaka, Lukobe, Butega. Nyamhongolo: Nyamadoke,Bujimile, Ibinza,<br><br>Iwelyashinga. Shibula: Mhonze A, Nyamwilolelwa, Kihili,<br><br>Shibula, Buganda, Masemele, Igogwe, Isanzu, |
| 55 (f) | Maji uchimbaji wa visima virefu, ujenzi wa mabwawa | Mradi wa kisima kirefu Kata ya Nyamhongolo uliojengwa kwa msaada wa Serengeti Breweries unaotumia solar, umekamilika na jumla ya kaya 7000 zimeanza kunufaika na mradi huo. |
| 55 (a) | **Maji taka;** Kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya uondoaji majitaka nchini na kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi. | Utekelezaji wa shughuli za mradi unaendelea na uko katika hatua za mwisho umefikia 80% ya utekelezaji, Mkandarasi alisaini MKataba tarehe 28 Oktoba 2016. Kazi zote za mradi zinatarajiwa kukamilika tarehe 15th March 2018 kwa gharama ya shilingi Bilion 1.54 |

**Mradi wa usafi wa Mazingira Jiji la Mwanza (Nyamagana na Ilemela)**

| Na | Maelezo | Hatua iliyofikiwa | Matarajio | Gharama ya mradi |
|---|---|---|---|---|
| 4.1 | Kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi ya milimani. Kazi za mradi ni ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoaji wa majitaka (simplified sewerage system). | ▪ Mkandarasi alisaini MKataba tarehe 28 Oktoba 2016.<br><br>▪ Utekelezaji wa shughuli za mradi unaendelea na uko katika hatua za mwisho ambapo asilimia themanini (80%) ya kazi za mradi zimekwishakamilika | ▪ Kazi zote za mradi zinatarajiwa kukamilika tarehe 15th March 2018. | ▪ Jumla ya Gharama za mradi ni TShs. Billioni 1.54 |

| Na | Maelezo | Hatua iliyofikiwa | Matarajio | Gharama ya mradi |
|---|---|---|---|---|
| 4.2 | Kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya Shule za msingi, songo mnara *"public place".* | ▪ Wakandarasi walisaini MiKataba tarehe 28 Oktoba 2016. | ▪ Kazi zote za mradi zimekwishakamilika tangu tarehe 30 Novemba 2017. | ▪ Jumla ya Gharama za mradi ni TShs. Billioni 4.28 |

## 10.1 CHANGAMOTO

Mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kuchelewa kwa Mchango wa Serikali katika miradi inayofadhiliwa na Taasisi za nje.

ii. Kutokuwepo kwa kasma na Fedha za kufidia hasa pale ambapo eneo la mwananchi linatwaliwa kwa shughuli za umma Mfano; *Eneo la mabwawa ya majitaka (Nyamhongolo) linahitaji kiasi cha* ***shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya fidia.***



***Eneo la Kilimahewa lililowekewa miundo mbinu ya maji safi na maji taka kwa ufadhiliwa benki ya dunia. Ni mradi wa kwanza wa majaribio duniani.***



*Moja ya familia kati ya familia 1000 zilizonufaika na mradi wa majaribio unaofadhiliwa na benki ya ummoja wa ulaya iliyojenga mlimani ambayounganishiwa miundombinu ya maji taka na maji safi katika eneo la Kilimahewa Kata ya Nyamanoro*

## 11.0 UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

### 11.1 ELIMU YA UJASIRIMIAMALI

Kwa kipindi kifupi cha uongozi tumeweza kutoa elimu ya ujasirimiamali katika vikundi jamii CBO`S zaidi ya vikundi 350 katika Kata zote 19. Elimu hii imewawezesha wananchi kujitambua, kuwa wabunifu, kutumia fursa zilizopo na kupata maarifa ya kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Jumla ya shillingi 12,300,000/= zilitumika ikiwa gharama za mafunzo, kugharamia vinywaji, Usafiri, malipo kwa wawezeshaji, vifaa na katiba kwa vikundi vyote vilivyo pata elimu katika Jimbo zima.

**BANGO KITITA LENYE KUONESHA ORODHA YA VIKUNDI NA MABALOZI WALIOPATA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI NA UONGOZI**

| NA | JINA LA KATA | IDADI YA VIKUNDI | IDADI YA WANACHAMA | IDADI YA MABALOZI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mecco | 82 | 1,320 | 98 |
| 2 | Nyakato | 34 | 670 | 186 |
| 3 | Nyamanoro | 62 | 247 | 40 |
| 4 | Kirumba | 150 | 361 | 78 |

| NA | JINA LA KATA | IDADI YA VIKUN-DI | IDADI YA WANA-CHAMA | IDADI YA MABALOZI |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Nyamhongoro | 42 | 158 | 96 |
| 6 | Kayenze | 36 | 108 | - |
| 7 | Kiseke | 67 | 207 | - |
| 8 | Buswelu | 48 | 269 | 195 |
| 9 | Pasiansi | 24 | 176 | 56 |
| 10 | Nyasaka | 1 | 57 | 129 |
| 11 | Kawekamo | Viongozi wa vikun-di 46 | | 50 |
| 12 | Kitangiri | - | | 195 |
| 13 | Shibula | 1 | | - |
| 14 | Ibungilo | 36 | 183 | 12 |
| 15 | Kahama | - | | - |
| 16 | Ilemela | - | | 120 |
| 17 | Buzuruga | - | | 115 |
| 18 | Sangabuye | - | | - |
| 19 | Bugogwa | - | | 33 |
| **JUMLA** | | **629** | **3,756** | **1,403** |

***NB: Idadi ya wanaChama Kata zingine inaonekana wachache kutokana na kutolipia vyeti vyao. Masomo yalitolewa bure lakini vyeti ilibidi kulipia kupunguza gharama za uendeshaji.***




***Moja ya zawadi zilizotolewa na vikundi vya ujasiliamali wa mwaloni wakimtaka Mbunge kuwa nahodha wa meli ya maendeleo Jimbo la Ilemela.***



***Moyo usio na shukurani hukausha mema yote, nimekubali kuwa nahodha wa MV Maendeleo, inayoongoza maendeleo ya Jimbo la Ilemela.***




***Akina mama wajasiliamali wa kikundi cha Twiga cha Kirumba Kati ambacho mbunge wa Jimbo ni mwanachama.***




***Zawadi ya picha kwa mbunge yenye ujumbe mzito ambao tafsiri yake ni kufanya kazi kwa bidi bila kilele, matokeo ya kazi yatafikisha ujumbe.***



***Moja ya semina za wajasiliamali toka vikundi mbalimbali vya kata ya Kirumba na The Intergrity Foundation kwa ushirikiano na The Angeline Foundation***

Natoa shukurani za pekee kwa Katibu wa Mbunge Comrade Kheri James aliyeratibu mafunzo haya tangu mwanzo, aidha niwashukuru sana wawezeshaji wote, Ndugu Suleimani Mathias

Mkurugenzi wa SUDAMA Investment na Ndugu Patric Tungu Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania women and Youth Social Organization (TAWESO) na Issack Mnyadi wa Integrity Foundation kwa ushirikiano wao mkubwa waliounesha wakishirikiana na Taasisi ya The Angeline Foundation, kwa majitoleo ya kufanya kazi hii kwa kujitolea zaidi ili kusaidia jamii. Mwenyezi mungu awabariki sana. Juhudi zinaendelea kuhakikisha Kata zote zifikiwe kikamilifu. Ombi kwa waheshimiwa Madiwani kutoa ushirikiano na msukumo kwa wananchi wao ili wanapopata taarifa washiriki kikamilifu.



***Dkt. Angeline Mabula (Mb) akitunuku vyeti kwa kikundi cha akinamama walio hitimu elimu ya ujasirimiamali katika Kata ya Kirumba.***

**11.2 UTOAJI MIKOPO KWA WANAWAKE NA VIJANA 10% YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

Kwa kipindi cha miaka miwili jumla ya vikundi 129 ***(Wanawake vikundi 82, Vijana 47)*** vilipata mikopo yenye ***Jumla ya shilingi 283,000,000***/=. Pamoja na wajasiliamali wengi kupewa elimu, lakini bado kuna hali ya woga kuchukua mikopo hii ambayo ina riba nafuu sana. Aidha wananchi wengi wanashindwa kutimiza masharti ya uundaji wa vikundi kutokana na kutoaminiana, hivyo kufanya uchukuaji mikopo kuwa wakusuasua,

## 11.3 Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake

Wilaya imefanikiwa kunzisha jukwaa la wanawake ambalo lina jumla ya wanaChama 153. Jukwaa hili linawaleta pamoja wanawake wajasiriamali wa Wilaya ya Ilemela.

### 11.3.1 Uwezeshaji kiuchumi kaya maskini

(a) **Uhaulishaji wa Fedha kwa kaya maskini**

Jimbo la Ilemela ni moja ya majimbo yanayotekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF

III. Mpango huu ulianza kutekelezwa Mwaka 2014 kwa utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini. Uhawilishaji wa Fedha ulianza Mwezi Julai, 2015 katika mitaa 69 kukiwa na walengwa 4807. Mpaka kufikia Disemba 2017 Jumla ya Tsh 2,843,467,524.28 zimepokelewa kwa ajili ya kuhawilishwa kwa kaya maskini na usimamizi katika ngazi ya Jimbo, Kata na Mitaa. Kaya zinazonufaika na mpango huu ni kaya 3912 kwa Mwaka katika jimbo.

### 11.4 MAFANIKIO YA MPANGO

i. Kuwawezesha wanafunzi 1,340 wa Shule za Sekondari na 4,421 wa Shule za Msingi kutoka kaya zinazonufaika kupata mahitaji muhimu ya Shule ikiwemo sare na vifaa vya Shule.

ii. Kaya 2,448 zimeanza kutekeleza shughuli za kukuza na kuongeza kipato cha kaya. Kati yake zenye biashara ndogo ndogo kaya 1073, ufugaji kaya 549 kilimo cha matunda na mboga mboga kaya 771 na ushonaji kaya 55.

iii. Kuziwezesha kaya kufanya maboresho ya makazi na hali ya lishe ili kukuza rasilimali watu kufikia malengo ya mpango.

iv. Kuunda vikundi 115 vya walengwa ili kuwajengea misingi ya kushirikiana katika uzalishaji na kukuza mitaji. (Ufugaji 27, Kilimo 22, Ushonaji 6, Biashara 36 Kuweka na kukopa 24).

### 11.5 UBORESHAJI WA MAISHA.

Kwa kutambua changamoto ya hali duni ya maisha katika baadhi ya maeneo ya jimbo letu, Mbunge kwa kutumia mahusiano yake na chuo cha YONGNAM cha Korea Kusini, ameanzisha mradi wa kuboresha maisha na kuwa na mji wa kisasa. Mradi huu utafanyika katika kijiji cha IHALALO Kata ya Sangabuye na IPONYABUGALI Kata ya Kayenze. Tayari wasimamizi wa mradi huu kutoka Korea ya Kusini wamekwisha ripoti Jimboni na wamefanya vikao na wananchi katika maeneo ya mradi.

Jumla ya wanakijiji 6 na watumishi 4 walipata fursa ya kuhudhuria mafunzo kwa wiki 2 nchini Korea ya Kusini. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi na uendeshaji wa mradi. Aidha, tumeanza kutekeleza Mpango huu kwa kuanza kujenga vyumba vya 8 vya madarasa ambapo jumla ya Tshs 54,000,000 zimetolewa na nchi ya Korea Kusini kwa ajili ya Kazi hiyo.



***Marafiki wamaendeleo kutoka Nchini Korea, wakizungumza na wanakijiji katika eneo la IHALALO Kata ya Sangabuye.***



***Katibu wa Mbunge Komrade Kheri James akimwelezea jambo mmoja wa wadau wa maendeleo juu ya eneo kutakapofanyika mradi.***




***Moja ya vikao na viongozi wa Kata ya Kayenze tukihamasisha ushiriki wa jamii katika mradi unaofadhiliwa na Jiji la Deagu Korea ya Kusini. Katika picha ni Katibu wa Mbunge Comrade Kheri James akitoa ufafanuzi wa jambo***

## 12.0 UJENZI WA CHAMA

### 12.1 USHIRIKI KATIKA VIKAO VYA CHAMA

Mbunge kwa kutambua kuwa kwa nafasi yake ya ubunge ni mjumbe wa baadhi ya vikao vya Chama kuanzia ngazi ya tawi, ameshiriki vizuri katika vikao vyote vya kikanuni anavyo alikwa anapo kuwa Jimboni na pale anapo pata mwaliko mapema anapokuwa mbali kwa shughuli za kiserikali. Aidha, amekuwa mshiriki mzuri katika vikao mbalimbali vya mabaraza na Jumuiya.

### 12.2 USHIRIKIANO NA CHAMA NA WANACHAMA

Mbunge katika kipindi cha miaka miwili 2015 hadi 2017, akiwa Mbunge wa Jimbo, ameweka utaratibu wa kuutarifu na kuushirikisha uongozi wa Chama kwa kila jambo analo fanya jimboni ikiwa ni pamoja na kumwandikia katibu wa CCM juu ya kazi zote zinazofanywa na ofisi yake. Ushirikiano huu unakwenda sambamba na kuwahusisha Makatibu wa CCM wa Kata na Viongozi wa Serikali za Mitaa katika shughuli zote zinazofanywa na  aidha na Mbunge, Katibu wa Mbunge au waratibu walioko katika kanda kwenye ofisi ya Mbunge.

### 12.3 MICHANGO NA UWEKEZAJI KATIKA CHAMA

Kwa kutambua kuwa jukumu la kujenga Chama ni jukumu la kila MwanaChama, Mbunge amekuwa mstari wa mbele katika kukiwezesha na kukisaidia Chama kutimiza majukumu yake kwa namna mbalimbali, kama ifuatavyo:-

i. Mbunge ametoa semina ya uongozi na ujasirimiamali kwa mabalozi wote wa CCM katika Kata 16 na amegharamia mafunzo na posho yaliyogharimu shilingi 12,300,000/= ikiwa ni gharama ya usafiri na viburudisho.

ii. Mbunge pia amefanya ujenzi wa maliwato/choo cha Wilaya yaliyo gharimu kiasi cha TShs. 1,000,000/= baada kilichokuwepo kuwa kibovu na hatari kwa matumizi.

## 13.0 HAMASA NA MICHEZO

Mhe. Mbunge ametoa motisha na hamasa kwa Kata tatu zilizo fanya vizuri kwa kuongoza kwa kura za CCM katika uchanguzi uliopita kwa kutoa zawadi ya ngo`mbe 6 na kuchangia kiasi cha Tshs. 3,200,000/= kwa Kata 16 kama mchango wa kuimarisha uhai wa Chama.

### 13.1 MICHEZO

Uundeshaji mashindano ya Jimbo Cup unalenga kuinua vipaji kwa vijana wetu. Ni azma ya mbunge kuhakikasha kuwa kila mwaka mashindano haya yanafanyika japokuwa 2017 hayakuweza kufanyika, hata hivyo maandalizi yote yalikuwa yamekamilika ikiwemo vifaa vya michezo ambavyo kwa ujumla wake viligharimu Sh. 17,950,000.00 n.k. Kwa mwaka 2016 mashindano yalifanyika na timu ya Bugogwa walishinda nakunyakua zawadi ya kwanza wakifuatiwa na Kata ya Ibungiro. Aidha mashindano ya UMISETA NA UMITASHUMTA naya yalifanyika na The angeline Foundation iliwezesha na Manispaa ya Ilemela iliinuka kidedea kwa kushinda michezo mingi na kutwaa vikombe zaidiya 7.

Pamoja na mashindano ya mpira wa miguu, lengo letu nikushirikisha michezo mbalimbali ikiwemo mchezo wa karata, muziki, ngoma za asili n.k juhudi zinafanyika ili michezo mingine pia ipate nguvu.



**Mabingwawa Jimbo Cup 2016 timu ya Bugogwa wakisalimiana na waamuzi pamoja na wapinzani wao timu ya Kata ya Ibungilo.**



***Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela akisalimiana na timu ya Kata ya Ibungilo iliyoingia fainal ya Jimbo Cup mwaka 2016 nakuchukua ushindi wa pili.***




***Kwa pamoja na uongozi wa Mpira Wilaya ya Ilemela tukishuhudia moja ya mashindano ya Jimbo Cup kanda ya Bugogwa. Kata hi indo walikuwa washindi kwa Mwaka 2016. Kutoka kushoto ni Juma Msaka katibu wa TFF Wilaya ya Ilemela, Mbunge wa Jimbo, Diwani wa Kata ya Bugongwa Mhe. Mashamba, Katibu wa Mbunge Komrade Kheri D.James na baadhi ya wanachi waliofika kushuhudia mpambano.***



*Mashabiki wa soka wakifurahia mechi ya fainali ya jimbo  cup 2016*




*Viongozi waliofika kushuhudia finali ya Jimbo cup 2016 kati ya timu ya Kata ya Bugogwa na Kata ya Ibungilo wakisalia baada ya ukaguzi wa timu kukamilika wakiongozwa na Dr Leonard Masale pamoja na viongozi mbalimbali wilaya ya Ilemela.*



***Baadhi ya zawadi zilizotolewa kwa washindi wa kwanza hadi wa tatu.***



***Timu ya wasicha ya Marsh academy moja ya timu za wasichana ambayo iko ligi daraja la kwanza ni moja ya timu ninazozisaidia ili kuinua vipaji kwa wanamichezo.***




***Timu ya walimbwende ya Miss Tanzania 2016 waliozuru Halmashauri katika Kampeni ya kuhimiza shughuli za maendeleo Jimboni.***




***Washiriki wa Miss Tanzania 2016 walifika kutembelea ofisi za Manispaa ya Ilemela ambapo Mbunge wa Jimbo kupitia taasisi yake ya The Angeline Foundation ilikuwa moja ya wadhamini wa mashindano hayo.***



***Mbunge wa Jimbo Dr Angeline Mabula akitoa nasaha kwa washiriki hao, baada yakupata nao chakula cha jioni Yatch Club, Mwanza na kuwaomba kuwa mabalozi wazuri wa Tanzania kwa yeyote atakae bahatika kulitwaa taji la Miss Tanzania.***



***Waacheni watoto waje kwangu!!***



***Pamoja na shughuli za maendeleo anazoshiriki mbunge jimboni, pia hayuko nyuma katika matukio mengine. Katika Picha Mbunge anatoa huduma ya chakula kwa waombolezaji wa moja ya msiba Jimboni***



***Mbunge Dkt.Angeline S.L.Mabula, akiwa na wajumbe wenzake katika mkutano mkuu wa CCM Taifa mjini Dodoma 23.11.2016 wakati wakumthibitisha mwenyekiti wa CCM Taifa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.***

Pamoja na shughuli zote za kuleta maendeleo ya Jimbo, Mbunge ameshiriki pia katika kutoa michango mbalimbali kuimarisha ama kuwezesha Chama na Jumuiya zake ngazi ya Wilaya na Mkoa. Katika kuthibitisha hilo michango kadhaa amechangia shughuli za Chama kama ifuatavyo:-

i. Amechangia ununuzi wa matairi ya gari la Chama ngazi ya Wilaya yenye thamani ya Shs 2,000,000/= ili kurahisisha shughuli za kiutendaji.

ii. Amewezesha kiasi cha shilingi 7,740,000/= ikiwa ni malipo kwa mawakala wote katika mitaa yote 171 wakati wa uchaguzi wa Serikali za mitaa 2014

iii. Amechangia Shs 1,000,000/= ili kufanikisha ujenzi wa jengo la CCM Wilaya ya Ilemela.

iv. Amegharamia zaidi ya 4,500,000/= katika vikao mbalimbali vya Chama na Jumuiya zake. Aidha, aliwezesha upatikanaji wa chakula kwa wajumbe wote wakati wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi, 2017

v. Ujenzi na/au marmaliwato/choo cha Wilaya yaliyo gharimu kiasi cha Shs 1,000,000/= baada kilichokuwepo kuwa kibovu na hatari kwa matumizi.

vi. Kugharamia kikao cha Halmashauri kuu maalumu baada ya uchanguzi na kiasi cha Shilingi 700,000/= zilitumika kama mchango wa kikao cha Halmashauri ya kikanuni.

NB: Pamoja na kugharamia shughuli za Chama, baadhi ya wananchi kadhaa walipata msaada toka kwa Mbunge jumla ya shilingi 4,700,000/= ili kukidhi haja zao, sehemu kubwa ikiwa ni gharama za Shule, gharama za matibabu, mitaji ya biashara ndogondogo n.k. Fedha zote hizi zimetolewa kupitia ofisi ya Mbunge. Michango mingine mingi ambayo amekuwa akitoa kwa namna mbalimbali katika ngazi za Kata na Jumuiya ili Chama chetu kiweze kusonga mbele.

## 14.0 MAHUSIANO NA JAMII

Katika kipindi hiki Mbunge ameendelea kuwa karibu kwa kujenga na mahusiano na Taasisi zote za Umma na binafsi pamoja na wadau wa maendeleo bila kuwasahau wananchi na viongozi ndani ya Wilaya. Jambo hili limesaidia sana kutimiza vyema majukumu ya Mbunge katika kuimarisha mahusiano na viongozi wengine. Aidha Mheshimiwa Mbunge amefanikiwa kuwaalika Bungeni Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wa dini wanaotoka katika Jimbo la Ilemela ili kwenda kujifunza na kuona ni namna gani Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linavyofanya kazi. Aidha Wahe Madiwani na Viongozi walijionea uwajibikaji wa Mbunge awapo Bungeni. Shukrani za dhati ziwaendee sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Uongozi wa Halmashauri na Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuwa Msingi imara wa mahusiano



***Mhe. Mbunge akiwa katika picha ya pamoja na waheshimiwa Madiwani, Viongozi wa dini na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Ilemela walipotembelea Bungeni Mjini Dodoma kwa mwaliko wa Mbunge***



***Kutoka kushoto ni Naibu Mstahiki Meya Mhe Shaaban Maganga, Katibu wa CCM wa Wilaya Komrade Achen Maulid, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ndugu Nelson Mesha, Dkt Angeline S. L. Mabula Mbunge wa Jimbo, Mstahiki Meya Mhe Renatus Mulunga, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Ndugu John Paul Wanga na Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji Mhe Alex Ngusa walipotembelea Bungeni kwa mwaliko wa Mbunge mapema 2016.***

## 15.0 ZIARA MBALIMBALI KATIKA JIMBO

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi, tumefanikiwa kufanya Ziara ya Kiserikali katika Kata zote 19, lengo la ziara hizo ilikuwa ni kusikiliza kero na kupokea maoni kutoka kwa wananchi. Watumishi wa Halmashauri wakiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa walishiriki kikamilifu katika ziara hiyo. Jambo la kufurahisha zaidi katka ziara ya kiserikali, Mkuu wa Wilaya Dkt. Leonard Masale alishiriki kikamilifu na kujibu hoja pale zilipojitokeza kugusa ofisi yake. Ziara ya kiChama nayo imefanyika lakini taarifa yake itaingia katika taarifa ya Mwaka 2018. Katika ziara hizi Mheshimiwa Mbunge aliambatana na Viongozi wa Halmashauri, Madiwani na Viongozi wa Chama wa ngazi ya Kata



***Pichani Mhe. Mbunge akiwa katika ziara akitoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na wananchi katika Kata ya Kawekamo. Kosoto kwake ni Diwani wa Kata Mhe Mashamba.***



*Moja ya mikutano ya hadhara katika Kata ya Nyakato*



16.0 **USHIRIKI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO**

Kauli mbiu ya Jimbo inasema Ilemela ni yetu Tushirikiane Kuijenga, kama mwana Ilemela, Mbunge ameshiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ziwe kidini au za kijamii ndani na nje ya jimbo. Aidha ushiriki katika vikao na shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwemo ziara za viongozi wa Kiserikali katika Jimbo lengo nikuhakikisha kuwa fursa inapojitokeza uwepo wa mbunge ni muhimu sana. Pamoja na ujenzi wa miundombinu kadhaa jimboni kwake, nimeshiriki mialiko mingi katika shughuli za kijamii. Jumla ya mialiko 105 nilipokea na kushiriki mialiko 52 tu mingine niliwakilisha kutokana na majukumu ya kikazi.




***Fursa mbalimbali za kimaendeleo zinapatkana katika jengo la biashara maarufu kama {Rocky City Mall}. Ni moja ya kivutio ambacho watu wanakuja kutembelea mara kwa mara***

17.0 **UWEZESHAJI**

Katika kuhakikisha kuwa utendaji wa Mbunge unakwenda sambamba na Madiwani, Mheshimiwa Mbunge amefanikiwa kuwezesha kufanyika kwa Semina muhimu na maalumu kwa Waheshimiwa Madiwani ambayo ililenga kuwajengea uwezo wa kumudu vyema majukumu yao na kuongeza ufanisi wa kazi. Semina hizo zimefanyika mara mbili katika Hoteli ya Njiwa Pori iliyoko wilaya ya Nyamagana na Mornach hotel iliyoko wilaya ya Ilemela Mwanza



***Waheshimiwa Madiwani wakiwa katika semina iliyoandaliwa na Hans Deal Foundation kwa maombi ya Mbunge wa Jimbo ili kuwaongezea maarifa juu ya masuala ya uongozi.***

## 18.0 OFISI YA MBUNGE

Ili kuboresha utendaji katika ofisi ya Mbunge, utaratibu wa utendaji ulibadilika kwa kufungua ofisi za kanda tatu, Kanda ya Kirumba, Bugogwa na Nyakato. Jambo hili haliko katika utaratibu wa ofisi za waBunge. Utaratibu huu umeleta ufanisi mkubwa kiutendaji kwa kuwafilia wananchi kwa wakati. Mtendaji mkuu katika ofisi ya Mbunge aliteuliwa Komrade Kheri Denice James akisaidiwa na waratibu wa Kanda Ndugu Rebeca Yusufu Kanda ya Bugogwa, John Makorosho Kanda ya Nyakato, Fatuma Kaloli Kanda ya Kirumba.



***Timu ya Wasaidizi Ofisi ya Mbunge Katibu wa Mbunge na Waratibu wa Kanda. Kutoka kushoto ni Ndugu Rebecca Anaeli Yusuph Mratibu kanda ya Bugogwa, Ndugu Fatuma Kaloli Mratibu kanda ya Kirumba, Comrade Kheri Denice James Katibu wa Mbunge, Ndugu John Makorosho mratibu kanda ya Nyakato, na Ndugu Mpunzi Mbegeje mratibu wa Wilaya***

## 19.0 KAULI MBIU YA JIMBO

Ili kuhamasisha umoja na kuharakisha maendeleo Mheshimiwa Mbunge ameanzisha kauli Mbiu isemayo ***'Ilemela ni yetu, tushirikiane kuijenga'*** Kwa hakika kauli Mbiu hii ndiyo umekuwa msingi mkubwa wa kuhamasisha shughuli za maendeleo na imetuvusha kwa kiwango kikubwa sana.

## 20.0 MAWASILIANO

Mhe Mbunge katika kati yake na Wananchi ilimlazimu kuboresha mawasiliano, kutenganisha shughuli za ofisi na zile za Jimbo hivyo, ililazimika kuanzisha namba maalumu ya simu ambayo inatumiwa na mwananchi yeyote kufikisha kero au ujumbe ofisi ya Mbunge. Namba hiyo ni 0624000888.

Vilevile, kuna barua pepe ya ofisi ambayo ni officeyambungeilemela@gmail.com. Aidha, ofisi imefungua pia._Ukurasa rasmi wa kijamii wa kuzungumza na wananchi kwa masuala yote yakijimbo.

Pamoja na njia zote hizo, redio za jamii pia hutumika kupeleka ujumbe kwa wananchi kupitia vipindi mbalimbali ambavyo tumekuwa tukifanya kwa lengo la kuwa habarisha na kuwa elimisha wananchi husasani wa Jimbo la Ilemela.

## 21.0 CHANGAMOTO

Pamoja na juhudi zote za kimaendeleo zilizofanyija Jimboni, bado kuna changamoto ambazo tunaendele kuzifanyia kazi, ukizingatia kuwa maendeleo ni mchakato usioweza kukamilika kwa mara moja bali ni hatua kwa hatua. Changamoto hizo ni pamoja na: Miundombinu ya barabara bado hairidhishi, Maji safi na salama bado ni tatizo katika baadhi ya maeneo, maeneo ya Vijijini 30%, eneo la mjini ni 90% ukosefu vitendea kazi, migogoro ya Ardhi bado ni changamoto, upungufu wa watumishi kwa kada zote n.k. Yote haya ofisi ya Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa bado tunaendelea kushughulikia

## 22.0 SHUKURANI

Mafanikio yote yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015 – 2020 yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya ofisi ya Mbunge, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Ofisi ya Mkuu wa wilaya, Ofisi ya Chama, Jamii ninayoiwakilisha na wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Jimbo. Nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliowezesha jimbo kufikia hatua tuliyo nayo, aidha siyo rahisi kumshukuru kila mmoja kwa jina lakini natambua msaada wao. Kwa uchache nitawataja wadau wamaendeleo waliokuwa bega kwa bega muda wote: WAZEE WAFANYA BIASHARA WA MWANZA, MAMLAKA YA MAJI SAFI NA TAKA MWANZA (MWAUWASA), SERENGETI BREWERIES, PSPF, LAPF, NHC, TIGO, AZANIA BANK, CRDB BANK, SIMU SOLAR, VITA FORM, NYANZA ROAD WORKS, NYANZA BOTTLING LTD, PEPSI, MWANZA HUDUMA, DUBAI BAZAAR, K.K LINK HOMES, BLACKWOOD DEVELOPERS, NITETEE FOUNDATION, SUDAMA INVESTMENT, INTERGRITY FOUNDATION, NA TANZANIA WOMEN AND YOUTH SOCIAL ORGANIZATION (TAWESO) TECNOSAVE, NIC, CWT, USHIRIKA WA WANAWAKE WAVUVI. Aidha wadau mmoja mmoja walioshiriki ni wengi tunawatambua kwa kuwa wako katika kumbukumbu zetu katika ofisi ya mbunge.

## 23.0 MATARAJIO

Taarifa hii imeanisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka miwili tangu nichaguliwe kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilemela nikitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020. Katika kipindi kilichobakia, nitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama ilivyo ada, ili kuhakikisha kuwa wananchi wa Jimbo la Ilemela wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na hawaachwi nyuma katika jitihada za Serikali ya awamu ya tano za Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati. Maendeleo ni mchakato tutaendelea kuhamasishana ili kila mmoja wetu awajibike katika kujenga uchumi wa taifa nawa mtu mmoja mmoja.

## 24.0 HITIMISHO

Ufanisi uliopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi yam waka 2015 – 2020, umetokana na mshikamano wa dhati ulipo kati ya ofisi ya Mbunge, Mkuu wa wilaya, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Ofisi ya CCM Wilaya, Waheshimiwa Madiwani na viongozi ngazi ya kata, Mitaa na Mashina, na Wadau mbalimbali wa Maendeleo. Kwa pamoja tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa, hivyo naendelee kuwaasa viongozi wenzangu tuendelee kuwa na mshikamano wa dhati, tukumbuke kuwa wote tunajenga nyumba moja hatuna sababu ya kugombea fito. *UMOJA NI NGUVU NA UTENGANO NI UDHAIFU,* Kamwe mtu asijione amesimama na ghafla akaanguka kwa kuwa tu alijihakikishia uimara kwa mambo mengi kumbe hana mizizi iliyojikita chini.

Kwa kipindi cha miaka miwili tumejitahidi kutekeleza ilani kwa kiwango kikubwa. Niwazi changamoto za Jimbo ni nyingi haziwezi zote kukamilika kwa muda mfupi. Rai yangu kwa viongozi wenzangu kila mmoja akitimiza wajibu wake tutafikia malengo ya taifa.

Aidha nawaomba viongozi wenzangu kuanzia kwa Balozi, Mwenyekiti wa Mitaa, viongozi wa chama ngazi ya tawi hadi wilaya, waheshimiwa Madiwani tushikamane kwa dhati kuwatumikia wananchi waliotupa dhamana ya uongozi. Tusinyoosheane vidole maana kila mmoja wetu kwa nafasi aliyochaguliwa anayo majukumu yakutekeleza. Tushirikiane kwa dhati katika kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda na kuwa na uchumi wa kati. Hali hiyo tutaifikia ikiwa tutazungumza lugha moja katika kuyachochea maendeleo jimboni kwetu na taifa kwa ujumla.

***MUNGU AWABARIKI SANA.***



*Ninawashukuru wananchi wa ILEMELA kwa kuniamini na kunipa fursa yakuwa mwakilishi wenu. Jambo moja ningependa kuwashirikisha, Maendeleo ni mchakato kila mmoja wetu anayo nafasi yakushiriki kikamilifu ili kufikia ndoto zake za maendeleo. Wana ILEMELA tunatakiwa kuwa na Dhamira moja, Uthubutu na daima kuwa wakweli na kukubali ukweli.* ***Ukweli utatuweka huru.***

**Jedwali Na.1**

**MATUMIZI YA FEDHA TOKA MFUKO WA "THE ANGELINE FOUNDATION"**

| NA | MATUMIZI | WANUFAIKA | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mafunzo ya ujasiliamali kwa vikudi | Kata 16 zilihudumiwa | 12,300,000.00 |
| 2 | Gharama za kukodi grader na kuweka mafuta | Miundombinu ya barabara | 13,717,000.00 |
| 3 | Gharama za maafa katika kata | Usafiri na rambirambi | 4,600,000.00 |
| 4 | Madawati 1923 ya shule za msingi | Kata zote zilipokea | 163,455,000.00 |
| 5 | Sementi mifuko 546 | Iligawanywa katika shule mbalimbali | 8,626,800.00 |
| 6 | Matofali 21,050 | Yaligawanywa katika kata | 16,840,000.00 |
| 7 | Misaada mbalimbali kwa wahitaji | Watu kadha waliofika kuomba ofisi ya mbunge | 4,730,000.00 |
| 8 | Ujenzi wa chumba cha maabara kituo cha afya Buzuruga | Kata ya Buzuruga, Mecco, Nyasaka,Nyakato n.k | 15,000,000.00 |
| 9 | Ununuzi wa vifa vya michezo, kwa ajili ya Jimbo Cup, UMISETA na UMITASHUMTA 2016/17 | Kata 19, Clubs 3 na timu za vijana 4, Shule za msingi na Sekondari | |
| 10 | Ununuzi wa vitabu 720 vya sayansi kwa shule 3 za Sekondari | Sekondari ya Ibinza, Kilimani na Mihama | 8,200,000.00 |
| **JUMLA** | | | **265,418,800.00** |

**Jedwali no 2**

**MGAWANYO WA VIFAA VYA UJENZI VILIVYOTOLEWA KUPITIA MFUKO "THE ANGELINE FOUNDATION"**

| NA | MTAA/KATA | SARUJI | BATI | MADAWATI | TOFALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kayenze | 5 | | 80 | |
| 2 | Sangabuye | 35 | 54 | 80 | 4,500 |
| 3 | Bugogwa | 40 | | 307 | 3,300 |
| 4 | Shibula | 20 | | 180 | 1,000 |
| 5 | Ilemela | 90 | 216 | 80 | 1,500 |
| 6 | Pansias | | | 140 | 3,500 |
| 7 | Ibungiro | 20 | 54 | 100 | |
| 8 | Kitangiri | 25 | | 80 | 1,500 |
| 9 | Nyamanoro | 26 | 32 | 160 | |
| 10 | Kirumba | | | 205 | 4,500 |
| 11 | Buswelu | 160 | 162 | 180 | 4500 |
| 12 | Nyamhongolo | 40 | | 80 | 3,500 |
| 13 | Kahama | 25 | | 80 | 3,500 |
| 14 | Kiseke | | | 80 | |
| 15 | Mecco | 40 | 108 | 80 | 1,800 |
| 16 | Buzuruga | 20 | 54 | 80 | 1,000 |
| 17 | Nyakato | | | 80 | 2,500 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 18 | Nyasaka | | | 80 | 4,250 |
| 19 | Kawekamo | | | 80 | 2,500 |
| | **JUMLA** | **546** | **720** | **1,923** | **40,850** |

**Jedwali Na. 3**

**MIUNDOMBINU ILIYOPATIKANA KWA MSAADA WA TAASISI YA "THE ANGELINE FOUNDATION"**

| NA | MTAA / KATA | SEKTA YA AFYA | SEKTA YA ELIMU | SEKTA YA MAJI | SEKTA YA BARABARA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Nyamhongolo | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 2 | Shibula | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 3 | Kirumba | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 4 | Mecco | | ✓ | | ✓ |
| 5 | Nyakato | ✓ | ✓ | | ✓ |
| 6 | Buzuruga | ✓ | ✓ | | |
| 7 | Nyamanoro | | ✓ | ✓ | ✓ |
| 8 | Ibungiro | | ✓ | ✓ | |
| 9 | Ilemela | | ✓ | | ✓ |
| 10 | Sangabuye | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 11 | Nyasaka | | ✓ | ✓ | |
| 12 | Kayenze | | ✓ | ✓ | ✓ |
| 13 | Bugogwa | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 14 | Kahama | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| 15 | Kitangiri | | ✓ | ✓ | ✓ |
| 16 | Kawekamo | | ✓ | | ✓ |
| 17 | Pansias | | ✓ | | ✓ |
| 18 | Kiseke | | ✓ | ✓ | ✓ |
| 19 | Buswelu | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

✓ *Miundo mbinu iliyojengwa katika kata husika*

**Jedwali Na. 4**

**MICHANGO MBALIMBALI YA MBUNGE KATIKA KUIMARISHA CHAMA NA JUMUIA ZAKE**

| NA | MAELEZO | CHAMA | UWT | WAZAZI | UVCCM |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la ofisi ya Chama na maliwato | 2,000,000/= | | | |
| 2 | Tairi za Gari la Chama | 2,400,000/= | | | |
| 3 | Gharama za vikao na mikutano | 5,200,000/= | 1,750,000/= | 1,000,000/= | 2,700,000/= |
| 4 | Sare za Chama | - | 550,000/= | | 6,250,000/= |
| 5 | Katiba za Chama | 350,000/= | | | |
| **6** | **Jumla** | **9,950,000/=** | **2,350,000/=** | **1,000,000/=** | **8,950,000/=** |

**Jedwali no 5**

**MATUMIZI YA MFUKO WA JIMBO KUANZIA 20015/2016 – 2016/2017**

| NA | MWAKA | MAELEZO/MATUMIZI | ENEO NUFAIKA | KIASI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **2015/16** | Utengenenezaji wa madawati 530 umefanyika katika shule za msingi | Shule za Msingi jimboni | 53,156,600.00 |
| 2 | **2016/17** | Kuchonga barabara ya kahama – Isela – Ihala-lo- isesa –Ngwangwila – Kayenze yenye urefu wa km 18.6 | Kahama _ Sangabuye - Kayenze | 44,500,000.00 |
| 3 | **2016/17** | Kujenga Kivuko | Mecco | 4,000,000.00 |
| 4 | 2016/17 | Ujenzi wa kivuli kwa ajili ya akina mama katika Zahanati ya Kirumba | Kirumba | 5,029,000.00 |
| **JUMLA** | | | | **106,685,600.00** |

**Pesa zilizopokelewa**

2015/2016 zilipokelewa Shilingi 53,156,000.00

2016/2017 zilipokelewa Shilingi 49,954,341.78

2017/2018 zilipokelewa Shilingi 59,726,000.00

**Jumla ya fedha zilizopokelewa Sh: 162,836,341.78**

**Fedha zilizobaki katika mfuko Sh. 56,150,741.00**

**Jedwali no 6**

**ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA VILIVYOPEWA MIKOPO MWAKA 2016/2017**

**Kata ya Nyasaka**

| Na. | Jina la Kikundi | Wanawake | Vijana | Mkopo uliotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nyasaka VICOBA | | | 2,500,000.00 |
| 2. | Hapa kazi tu – 2015 | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Juhudi Youth | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Tupendane Group Nyasaka | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | SMWAWATA | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Umoja wa VIWANYASA | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Nyasaka Mazingira Group | ✓ | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Umoja wa Nyota Njema | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 9. | Tuinuane group Nyamuga | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **18,500,000.00** |

**Kata ya Buzuruga**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Umoja wa Vijana Ustawi | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 2. | Mshikamano Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Bodaboda Group Kata ya Buzuruga | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Women Trust Buzuruga | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Kikundi cha Wajane waishio Nyakato | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Motomoto Ustawi | | | 2,000,000.00 |
| 7. | Tufanikiwe pamoja group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Urafiki Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Kitangiri**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Tuinuane Group 2016 | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Muungano Goup | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Mwanza Sanaa Troupe | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Maendeleo Group Kitangiri Kati | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Upendo Jiwe Kuu | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | VIWAPIKI | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | Twaweza Group 2016 | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 8. | Umoja ni Nguvu 2016 | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Bugogwa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Akina Mama Wapalanganaji- Bugogwa | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Youth Development | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Tupendane Mama | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | HIMAJA Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Kikundi cha Hisa Furaha | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Umoja wa vijana Igombe | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | Mshikamano Bugogwa | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **14,000,000.00** |

**Kata ya Ilemela**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kikundi cha Faraja Lumala Mashariki | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Vijana Kazi ni Kazi | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Umoja wa Waendesha Pikipiki | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Upendo Group Butuja | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Tupendane Women Group Sabasaba | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Balimi Basukuma Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Nsumba Ntale Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 8. | Umoja wa Matawi group Lumala | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Kirumba**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | UWAWAKI | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Tushirikiane Bodaboda Kirumba | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Mshikamano Kirumba | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Nguvu Kazi na Maendeleo | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | Amani | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Umoja wa Vijana Amani | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | Tujikwamue ibanda ziwani | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Amani Mteremko Kirumba | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Kayenze**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fara Kayenze | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Victoria B Kayenze | ✓ | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Akina mama na Maendeleo Bezi | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Kikundi cha VICOBA | | | 2,000,000.00 |
| 5. | Umoja wa vijana wajasiliamali | | | 2,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | Usafi wa mazingira Bezi | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **12,000,000.00** |

**Kata ya Ibungilo**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Akina mama Ibungilo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Ukweli na Uwazi | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Umoja wa Maendeleo Group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Daneta | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Kundi la Tufashanywe | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Muungano wa Wajane Nyamanoro | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **12,000,000.00** |

**Kata ya Nyamhongolo**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Tusaidiane Mayelu | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Mkapa Kwaya | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Kitongoji cha Ikigilo | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 4. | Mushikamano Kaguha | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | Majiko Sanifu Nyamadoke | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Witogwa Ibinza | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | WABONYAC | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Wanakazi | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Kiseke**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wasukuma VICOBA Group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 2. | Jipe Moyo Zenze | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Tupendane Nsumba | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Amani na Upendo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | VIWABOKI Kiseke | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Mwamko | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **12,000,000.00** |

**Kata ya Kahama**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wanawake tuinuane Mtaa wa Wilunya | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Akina mama Ebenezer | ✓ | | 2,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Upendo Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Umoja wa Vijana Buyombe | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | Mshikamano Buyombe | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Wanawake Ujirani mwema Buduku | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Mapendo Vicoba Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 8. | Alfa na Omega | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Kawekamo**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Neema Yatosha Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Wanawake Ngwigwano | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Mshikamano Kawekamo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Kikundi cha Fram | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Pamoja Tunaweza Group Nyasaka A | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Amani Group 2016 | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Amani na Upendo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **14,000,000.00** |

**Kata ya Pasiansi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Umoja wa Waendesha Pikipiki | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 2. | Mshikamano Bwiru | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Umoja wa Akinamama Pasiansi Chini | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Umoja wa Vijana Pasiansi Polisi (UVPP) | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | Umoja wa Vijana Mnarani (UVM) | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Maliasili Women Group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | Hekima Group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Kikundi cha kujikomboa | | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,000,000.00** |

**Kata ya Buswelu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Umoja wa Vijana Maendeleo | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 2. | Madereva wa Malori | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Akina Mama Wajasiriamali Mbogamboga | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Umoja wa Akina mama Manispaa ya Ileme-la (UWAMI) | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Wapiganaji | | | 2,000,000.00 |
| 6. | Imani Kigala | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 7. | Kikundi cha Maendeleo Buhyila | ✓ | ✓ | 2,000,000.00 |
| 8. | Akina Mama Bunyanya | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 9. | Agano Joshoni | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 10. | Twins Busenga | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 11. | Songambele Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 12. | Wasamaria Bulola B Buswelu | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **24,000,000.00** |

**Kata ya Nyakato**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Akina mama Tupendane – Ihangilo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Nyakato Umoja Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 3. | Muungano Akina Mama National Maghari | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Mshikamano Group | | | 2,000,000.00 |
| 5. | Agape group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 6. | Kimana | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Muungano Kangaye 'A' | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | ✓ | | **14,000,000.00** |

**Kata ya Nyamanoro**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mwamko VICOBA Sustainable | ✓ | | 2,500,000.00 |
| 2. | Amani Mkudi | ✓ | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Upendo Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Kikundi cha Faraja Mnyampala B | | | 2,000,000.00 |
| 5. | Nuru njema | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Amani Kilimahewa | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Umoja wa Mafundi maduka mawili | ✓ | | 2,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | Wanawake Mwongozo | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **16,500,000.00** |

**Kata ya Mecco**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Teremendous | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 2. | Umoja Group Mecco | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Kikundi cha kuleana Mecco | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Akina mama Mshikamano Mecco | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 5. | Wachapakazi Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 6. | Songambele | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 7. | Amsha amsha Nzengo A | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **14,000,000.00** |

**Kata ya Sangabuye**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Masaligula Group | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Wakereketwa wa CCM Hisa group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Akina Mama Tujengane Sangabuye | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Kikundi cha Wanawake Tukomboane | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Kikundi cha UWI Ilekako | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **10,000,000.00** |

**Kata ya Shibula**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Umoja wa Akina Mama Nyamwilolelwa | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 2. | Mhonze Vijana Group | | ✓ | 2,000,000.00 |
| 3. | Kikundi cha Twiyambilije | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 4. | Mshikamano Buganda | ✓ | | 2,000,000.00 |
| 5. | Mshikamano | ✓ | | 2,000,000.00 |
| | **Jumla** | | | **10,000,000.00** |



*Mwenyekiyi wa CCM taifa Dr Jakaya Mrisho Kikwete na mgombea urais Dr John Pombe Joseph Magufuli kwa pamoja wakinadi wagombea ubunge jimbo la ilemela na Nyamagana Angelina Mabula na Stanslaus Mabula wakati wa kufunga kampeni za uchaguzi mkuu wa taifa uwanja wa CCM kirumba tarehe 24.10.2015*